# Nipashe

Alhamisi Oktoba 8, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580362

www.ippmedia.com

The Guardian digital   nipasheTZ   nipasheTZ   nipasheTZ   0745 700710




**JAJI MKUU:** Mahakama tumejipanga kusikiliza kesi za uchaguzi mkuu

UKURASA 3



**WATU** saba mbaroni tuhuma za mauaji mlinzi wa bilionea

UKURASA 3

**WAFUASI** CHADEMA matatani kwa madai ya kufanya vurugu

UKURASA 4

# KARIBU ZAIDI



Rais John Magufuli akimlaki Rais wa Malawi, Dk. Lazarus McCarthy Chakwera, akiwa na mkewe, Monica Chakwera, walipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana, kuanza ziara ya siku tatu ya kiserikali. **PICHA: IKULU**

## JPM, Rais Malawi wakubaliana kushirikiana uchukuzi, kilimo, uvuvi, madini na utalii...

*Endelea Uk. 2*


# FURSA

## Mawakala wa uuzaji Magazeti



Kampuni ya **THE GUARDIAN LIMITED.**
Inakutangazia ya kuwa inatafuta mawakala wa wauzaji wa magazeti yake nchi nzima.kama unafahamu Biashara , au umeshawahi kufanya biashara unakaribishwa unatakiwa uwe na vitu vifuatavyo;

- Amana ambayo itafafanuliwa kutokana na idadi ya magazeti utakayohitaji
- Uwe na wauzaji (Vendors)
- Kitambulisho cha uraia
- Barua ya Mdhamini.
- Barua ya utambulisho wako kutoka kwa Mwenyekiti wa Serikali ya mitaa unapoishi.
- Barua ya utambulisho ya Mdhamini wako kutoka kwa Mwenyekiti wa serikali ya mitaa
- Picha 2 za Muombaji

Hii ni fursa ya kupata faida kubwa kwa kila nakala moja ya gazeti utakayouza.

Kwa Maombi na Ufafanuzi zaidi Wasiliana nasi

Meneja Usambazaji na Masoko
Mikocheni Light Industrial Area
S.L.P 31042, Dar es Salaam, Tanzania
Namba :+255716500500
Barua Pepe:circulation@guardian.co.tz
Mwisho wa Maombi ni 13 Oktoba 2020


## Magufuli ampigia Zitto kumpa pole

UKURASA 2



UKURASA 2

## Lissu apanda mwendokasi, anunua bidhaa Kariakoo

**MICHEZO** YANGA YASHUKURU DABI KUAHIRISHWA UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6


**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

# Magufuli, Rais wa Malawi wakubaliana kushirikiana

**Christina Mwakangale na Zainab Rashid**

TANZANIA na Malawi zimekubaliana kushirikiana kuboresha sekta za usafirishaji, uvuvi, madini, nishati, utalii na kilimo.

Makubaliano hayo yalitangazwa jana Ikulu jijini Dar es Salaam wakati wa hafla maalum iliyohusisha marais wa nchi hizo mbili, mwenyeji Dk. John Magufuli na Rais Lazarus Chakwera aliyezuru nchini kwa ziara ya siku tatu.

Rais Magufuli alimshukuru Rais Chakwera kwa kuitembelea Tanzania na kuwa nchi ya tatu kutembelewa barani Afrika kwa kiongozi mpya wa Malawi baada ya Burundi na Uganda tangu aingie madarakani.

"Biashara ya Malawi na Tanzania imepanda ilikadiriwa kuwa Dola za Kimarekani milioni 60 mwaka 2015 hadi milioni 80. Nia ni kutaka biashara ipande zaidi.

"Malawi ni marafiki zetu wakubwa, historia imeanza tangu tukiwa chini ya wakoloni, hata baada ya kupata uhuru chini ya Kamuzu Banda na Mwalimu Nyerere.

"Hata aliyepandisha bendera Mlima Kilimanjaro mwaka 1961 anaitwa Nyirenda, asili yao ni Malawi, wapo pia kina Mwanisongole nchi zote, undugu upo," alisema.

Rais Magufuli alisema kuna kampuni nane kutoka Malawi zimewekeza nchini na kutoa ajira kwa Watanzania 390 na kwamba zipo kampuni zilizowekeza Malawi kutoka nchini.

Alisema usafiri ukiimarika baina ya nchi hizo mbili, utafanya biashara ifanyike kwa urahisi na hivyo nchi hizo zijiikite kwenye uhusiano wa kibiashara na mizigo ya Malawi kupitia Tanzania itaongezeka.

"Bandari ya Mtwara sasa inafanyiwa ukarabati mkubwa na kwa sasa ina uwezo wa kubeba tani 400,000, ikifika Desemba mwaka huu, itakuwa na uwezo wa kubeba tani milioni moja," alisema.

Rais Magufuli aliiagiza Mamlaka ya Bandari (TPA) kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa kipindi cha siku 60, kufungua ofisi zao Lilongwe, ili kurahisisha shughuli za usafirishaji kupitia bandari nchini.

Aligusia pia uzalishaji wa umeme katika Kituo cha Songwe, akisema wakijadiliana pamoja, gharama zitapungua kutokana na nchi ya Malawi kuwa na mahitaji makubwa ya umeme.

"Mahitaji ni megawati 400, lakini uzalishaji ni MW 380 na wakati wa kiangazi hushuka hadi MW 180. Sisi Tanzania tutakuwa karibu na megawati 5,000, tumezungumza na Mheshimiwa Rais kwamba zingine tutawapatia wakati tukisubiri maendeleo ya mradi wa Songwe," alisema.

Rais Magufuli alisema Malawi ikitaka kuanzisha zao jipya, Tanzania iko tayari kushirikiana nao, akibainisha kuwa Rais Chakwera ameamua kuanzisha kilimo cha korosho.

Awali, Rais Chakwera alisema bandari za nchi hizo mbili zikishirikiana, itasaidia kukuza uchumi wa nchi hizo.

"Ninayo furaha kubwa na ninashukuru sana kwa namna ambavyo mimi na ujumbe kutoka Malawi tumepokewa, ninahisi tupo nyumbani. Mheshimiwa Magufuli na mimi tumekuwa na mazungumzo ya muda mrefu.

"Tunataka wafanyabiashara wa nchi zetu washirikiane na Rais Magufuli amesema Wamalawi wasijisikie kama wapo mbali na bahari," alisema Rais Chakwera.

Alisema Malawi imejifunza kwa Tanzania na kuona ambavyo nchi za Afrika zinaweza kujitegemea na kukuza uchumi wa watu wake.

"Tunataka tujifunze kusimamia utekelezaji wa miradi ili tusitegemee sana nchi nyingine. Mungu ametupa rasilimali za kutosha ili kuendeleza mataifa yetu, pia tunataka kurahisisha usafiri wa watu na mizigo mipakani," alisema.

Rais Chakwera pia alieleza kuguswa kwa namna Tanzania ilivyodhibiti sekta ya madini na kuongeza mapato yake, akisisitiza ni mfano wa kuigwa.

"Tumefanya utafiti katika nchi yetu Malawi, tumeona kuna vito vingi vya thamani, lakini Malawi imekuwa hainufaiki na madini hayo, tunaona Malawi inufaike na madini hayo. Tunataka watu wasije nchini kwetu na kwenda kuvichakata vito vyetu na kuja kutuuzia, tutengeneze ndani ya Afrika," alisema.

Rais huyo alisema Malawi inahitaji kuboresha biashara kupitia Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), akisisitiza pia nchi za Afrika kuimarisha demokrasia kwa kufanya uchaguzi bila waangalizi wa kimataifa.

"Wanapokuja waangalizi hawa huja na taarifa ambazo wanazitoa wenyewe, tunaamini kwamba Afrika inaweza kuimarisha demokrasia yake na kuhakikisha taasisi zake zinafanya kazi vizuri," alishauri.

## JPM ampa pole Zitto

**Na Waandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, ametuma salamu za pole kwa Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, aliyepata ajali juzi mchana, mkoani Kigoma.

Kwa mujibu wa taarifa iliyorushwa kwenye akaunti ya Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, rais amtakia afya njema kiongozi huyo, ambaye alikuwa kwenye safari za kampeni mkoani Kigoma.

"Rais amepiga simu na kumpa pole, Zitto Kabwe aliyepata ajali mkoani Kigoma, ameomba heri apone haraka na anawashukuru madaktari na wauguzi wa Kituo cha Afya cha Kalya na Hospitali ya Maweni, kwa msaada walioumpa," ilisema taarifa hiyo.

Jana, Ofisa Habari wa ACT-Wazalendo, Arodia Peter, alisema Zitto alipata ajali akiwa na watu watano na wote walikuwa salama licha ya majeraha madogo madogo.

Naye Zitto katika ukurasa wake wa Twitter, aliandika; "Ninaendelea vizuri ilikuwa ajali mbaya sana, namshukuru Allah kwa kutuponya, shukrani wahudumu wa Kituo cha Afya Kalya, licha ya changamoto za huduma ya kwanza imetusaidia, shukrani madaktari na wahudumu Hospitali ya Maweni Kigoma, mimi na wenzangu mpaka sasa ni wazima."

Akizungumzia ajali hiyo, Zitto alisema gari yake liligongwa nyuma na gari jingine kisha likapoteza uelekeo na kupinduka zaidi ya mara mbili.

**■meandikwa na Zainab Rashid, Evelyneneema Ernest (SJMC) na Frank Maxmillian (TUDARCo)**



Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu (mwenye kofia kulia), akinunua matunda kwa ajili ya mahitaji ya nyumbani katika eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tundu Lissu apanda mwendokasi jijini Dar es Salaam

**Na Romana Mallya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amepanda usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka, akisema kuwa ili uwe bora zaidi, unatakiwa kuwa na mfumo wa usafirishaji mkuu wa Dar es Salaam.

Lissu alipanda usafiri huo jana kuanzia Kinondoni B hadi Gerezani, Kariakoo na kusema ilikuwa mara yake ya kwanza kuutumia usafiri huo.

Akiwa ndani ya basi, Lissu aliwauliza baadhi ya abiria kuhusu usafiri huo na wengi wao walionyesha kufurahishwa nao kutokana na kuwarahisishia kuwahi wanakokwenda.

"Hii ni mara yangu ya kwanza kupanda mwendokasi, ni mfumo mzuri wa usafiri, lakini unahitaji kuwa ndiyo mfumo wa usafiri wa mabasi katika jiji kubwa kama hili la Dar es Salaam," Lissu alisema baada ya kushuka kwenye mwendokasi.

"Miji mikubwa duniani huwa na kampuni za mabasi ya aina hiyo moja au mbili. Ili uwe bora zaidi, unahitaji uwe mfumo wa usafirishaji mkuu wa Dar es Salaam," alishauri akisisitiza kuwa mfumo huo ukiachwa peke yake, hautatosha kwa sababu jiji hilo linahitaji usafiri wa abiria wa reli katikati ya mji.

Lissu pia alishauri kwamba, kwa kuwa Dar es Salaam iko kwenye ukanda wa Bahari ya Hindi, inaweza kutumia usafiri wa majini kwa kuwa na boti kutoka Bunju mpaka Bandarini na Kigamboni hadi Bandarini ili kutatua tatizo la msongamano wa magari barabarani.

"Abiria niliozungumza nao ndani ya mwendokasi wameniambia wanaufurahia usafiri huu, lakini unawasaidia watu wachache kwa sababu hauendi kila mahali," alisema.

Mtaalamu huyo wa sheria alisema Jiji la Dar es Salaam lenye zaidi ya watu milioni tano, halina mahali ambako watu wanaweza kwenda kupumzika.

"Majiji makubwa duniani huwezi kutembea kilometa tano usikute eneo la wazi lenye miti na maji, watu wanahitaji eneo la kupumzika," alisema.

Lissu baada ya kushuka kwenye mwendokasi eneo la Gerezani, Lissu alikwenda hadi soko kuu la vyakula Kariakoo na kununua baadhi ya bidhaa ikiwamo matunda.

# Mahakama yajipanga kwa kesi za uchaguzi

**Na Hellen Mwango**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amesema mahakama imejipanga kushughulikia kesi za uchaguzi, endapo zitafunguliwa baada ya uchaguzi mkuu unaotarajiia kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Kadhalika, alisema Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), kimeshatoa mafunzo kwa majaji wa Tanzania Bara na wa Mahakama Kuu Zanzibar pamoja na Mahakimu Wafawidhi namna ya kushughulikia kesi za uchaguzi na kuandika hukumu.

Kauli hii aliitoa jana jijini Dar es Salaam, wakati akifungua mafunzo kwa wajumbe wapya wa Baraza la Chuo cha Uongozi wa Mahakama yaliyoandaliwa na IJA.

"Maofisa waliopatiwa mafunzo ya kushughulikia kesi za uchaguzi ujao ni pamoja na Majaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji Mkuu wa Zanzibar, Majaji wa Mahakama Kuu Tanzania na Zanzibar, Wasajili na Warajisi kutoka Mahakama ya Zanzibar, Mahakimu Wakazi Wafawidhi kutoka Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya," alisema Jaji Prof. Juma.

Alisema mafunzo hayo yameiweka mahakama ya Tanzania katika utayari wa kuendesha kesi za uchaguzi.

"Kama kutafunguliwa mashauri mbalimbali ya uchaguzi basi, mahakama imejipanga kukabiliana nayo kwani pamoja na mafunzo ya kuendesha mashauri hayo, lakini majaji na mahakimu wamefundishwa namna bora ya uandishi wa hukumu," alisema.

Aidha, alisema chuo hicho kinashiriki vyema katika kuleta mabadiliko makubwa ya kiutendaji yaliyokusudiwa kwenye mahakama kupitia Mpango Mkakati wa Mahakama wa miaka mitano na programu ya maboresho, ili kutimiza dira ya haki sawa kwa wote na kwa wakati.

Jaji Profesa Juma alisema licha ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na mahakama katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji haki, bado matumizi yamekuwa madogo kuliko ilivyotegemewa.

"Ingawa uongozi wa mahakama kwa takribani miaka mitatu sasa iliamua matumizi ya TEHAMA kuwa si hiari, lakini kwa bahati mbaya bado matumizi yake ni madogo kulinganisha na uwekezaji mkubwa uliofanywa. Huu ni wakati wa chuo kujiimarisha, ili kitoe mafunzo kwa watumishi wa mahakama kwenye eneo la utoaji haki mtandao," alielezea.

Naye Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, Jaji Paul Kihwelo, alisema mafunzo hayo yatafanyika kwa siku mbili na yanalenga kuwajengea wajumbe hao uwezo wa kutekeleza majukumu yao ikiwamo kusimamia utendaji wa chuo.



Bilionea Saniniu Laizer pamoja na viongozi wa dini wakifanya maombi maalumu katika eneo la mgodi wake, uliopo Mererani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, jana, sehemu ambayo mlinzi wake, Manase Wiliam, aliuawa kikatili hivi karibuni. Maombi hayo ni ya kulaani kitendo hicho na kutaka aliyehusika apatikane. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# 7 mbaroni tuhuma mauaji ya mlinzi mgodi wa Laizer

**Na Woinde Shizza**, SIMANJIRO

JESHI la Polisi mkoani Manyara, linawashikilia watu saba wakiwamo wafanyakazi wa mgodi wa madini ya tanzanite unaomilikiwa na Bilionea Saniniu Laizer, wakituhumiwa kuhusika na mauaji ya mlinzi wake, Manase William (47).

Wakati jeshi hilo likichukua hatua hiyo, Bilionea Laizer ameitisha maombezi maalumu katika eneo alilouawa mlinzi wake huyo, akimwomba Mungu kuwaumbua waliotekeleza unyama huo wakamatwe.

Manase alikutwa ameuawa katika lindo lake alfajiri ya Septemba 27, mwaka huu na mwili wake ulifanyiwa uchunguzi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru Oktoba 3 mwaka huu.

Maombi hayo yalifanyika jana katika mgodi wa Laizer ulioko Mirerani, mkoani Manyara.

Maombi hayo yaliwahusisha wafanyakazi wote wa mgodi huo maarufu kama 'Wana Apolo', huku Bilionea Laizer kushika udongo wa mahali, ambapo mlinzi huyo alikutwa ameuawa.

"Nimeamua kufanya maombi haya na wafanyakazi wangu, ili kama kuna waliohusika wapo hapa, waumbuke mapema na serikali iweze kuchukua hatua mapema," alisema Laizer.

Akiongoza ibada hiyo, Mchungaji Joshua Laizer wa Usharika wa Mirerani wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Meru, alisema tukio hilo ni baya na linapaswa kulaaniwa na kila mtu na kumwomba Mungu awaonyeshe aliyetenda ulahifu huo wa kinyama ndani ya siku saba, ili sheria ichukue mkondo wake.

"Damu ya Manase inalia hapa ardhini, tutashika udongo huu mahali damu yake ilipomwagika. Sisi hatumjui aliyemuua, tunamwomba Mungu atuonyeshe ndani ya siku saba, wauaji ni kina nani na wakamatwe," alisema Mchungaji Joshua.

Akinukuu maandiko matakatifu ya Bibilia, alisema mlango wa 27 wa kitabu cha kumbukumbu la Torati, mstari 24 na 25 unasema na 'alaaniwe mtu yeyote ampigaye mwenzake kwa siri na alaaniwe yeyote atakayemuua mwenzake pasipo na kosa".

Baada ya ibada hiyo, Bilionea Laizer alisema maombi hayo yanamlenga mtu aliyetenda tukio hilo baya na la kinyama kwa kusababisha kifo cha Manase, ili Mungu amwonyeshe hadharani na sheria ichukue mkondo wake.

Huku akionekana mwenye kuhuzuni, Laizer alisema ameumizwa na tukio hilo, ambalo halikuwahi kutokea katika mgodi wake na ndiyo maana ameamua kufanya maombi hayo ya kulaani tukio hilo lisijirudie tena.

"Marehemu aliajiriwa na mdhamini wa mgodi wangu, na hana muda mrefu tangu aanze kufanya kazi hapa.

Alikuwa kijana mwema, hana makuu na mtu yeyote, ila mimi ninaamini aliyehusika siyo mtu wa hapa ndani, atakuwa ametoka nje na eneo langu la mgodi.

"Mimi ninamwamini Mungu na mali ninayoipata inatokana na maombi ya imani yangu. Kwa hiyo, ninaamini kwa kupitia maombi haya, mhusika wa tukio hilo atapatikana. Sasa ninamwachia Mungu," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi Paul Kasabago, alisema hadi sasa jeshi hilo linawashikilia watu saba wakiwamo baadhi ya wafanyakazi wa Laizer, ambao wanahusishwa na tukio hilo.


Helium One

TATHMINI YA ATHARI ZA MAZINGIRA NA JAMII

TAARIFA YA AWALI YA MRADI TARAJIWA WA UTAFUTAJI GESI YA HELIUM KWA NJIA YA UCHORONGAJI KATIKA WILAYA YA MOMBA, MKOA WA SONGWE-

2159259O2

Kampuni za Gogota (Tz) Limited na Njozi (Tz) Limited zinamiliki leseni za utafutaji wa madini katika vitalu vyenye jumla ya kilomita za mraba 4,192.7 katika eneo la mashariki mwa bonde la Rukwa, kusini mwa Tanzania. Kampuni hizi zinataka kujiridhisha kuhusu uwepo wa gesi ya Helium. Gesi hiyo inatarajiwa kuwa na kiwango cha kati ya asilimia 4.2 na 10. Kabla ya mradi wa uzalishaji gesi kutekelezwa tafiti mbalimbali zimepangwa kufanyika na kati ya tafiti hizo ni tafiti kwa njia ya uchorongaji. Jumla ya visima vinne vinatarajiwa kuchorongwa katika maeneo mbalimbali ya mradi. Baada ya kumalizika kwa utafiti, visima hivi vitafunikwa mpaka pale uzalishaji utakapoanza.

Utafiti huu unatarajiwa kufanyika katika Kata za Kamsamba, Ivuna, na Mpapa katika Wilaya ya Momba, Mkoa wa Songwe. Uchorongaji unatarajiwa kuanza mwezi wa pili 2021 na unatarajwa kumalizika ndani ya miezi minne. Kwa mantiki hiyo kampuni za Gogota (Tz) Limited na Njozi (TZ) chini ya kampuni ya Helium One zimepanga kufanya tafiti hizi za athari zinazoweza kutokana na uwepo wa mradi huu kwenye mazingira na kijamii. Hivyo basi maombi ya kufanya tathmini hii yamefanywa kwa pamoja kati ya kampuni hizi mbili za Gogota (TZ) Limited na Njozi (TZ) Limited, hivyo cheti cha mazigira kitatolewa kwa Gogota (TZ) Limited na Njozi (TZ) Limited.

Kwa mujibu wa sheria za usimamizi wa mazingira kipengele namba 20 ya mwaka 2004, na sheria nyenza ya udhibiti na ukaguzi wa mazingira ya mwaka 2005, na marekebisho yake ya mwaka 2018, taarifa hii inawasilishwa kuufahamisha umma kwamba kampuni ya MTL Consulting Limited imepewa kazi ya kufanya tathimini ya athari za mradi huu wa uchorongaji wa visima kwenye mazingira na jamii kwa niaba ya kampuni za Gogota (Tz) Limited na Njozi (TZ). Tathmini hii itafanyika katika kata tatu zitakazojumuisha vijiji vya Kamsamba, Mkonko, Usoche, Mpapa, Masanyita, Kasanu, Lwatwe, Samang'ombe na Itumbula.

Taarifa hii inachapishwa ili kukusanya maoni, maswali, na ushauri kutoka kwa wadau wote wa mradi. Mdau yeyote mwenye maoni au taarifa yoyote juu ya athari zinazoweza kusababishwa na mradi huu kwenye jamii na mazingira awasiliane au atume maoni yake kwenye ofisi zifuatazo:

| | | |
|---|---|---|
| Mkurugenzi<br>Gogota (Tz) Limited and Njozi (Tz) Limited.<br>Gorofa ya Pili, Kilwa House, 369 Toure Drive, Oyster Bay<br>S.L.P 62, Dar Es Salaam,Tanzania<br>Mawasiliano+255 22 2600594 | Mkurugenzi Mkuu<br>Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC)<br>Ofisi ya Kanda ya Magharibi,<br>NSSF MAFAO House, Gorofa ya Kwanza<br>S.L.P 974, Kigoma/Ujiji, Tanzania.<br>Mawasiliano:+255-788825359<br>Barua pepel:.nemckigoma@nemc.or.tz | Meneja Mkuu<br>MTL Consulting Company Limited<br>Masaki, Nyumba namba 2,Kitalu 689<br>Barabara ya Sandvik<br>S.L.P 77894<br>Dar es Salaam, tANZANIA<br>Simu ya Mezani: *+255 22 2600594,*<br>*Simu ya mkononi: +255 767 360 225*<br>Barua pepe:info@mtlconsulting-tz.com |

# Wakamatwa kwa tuhuma kupanga kufanya uhalifu

**Na Samson Chacha,** TARIME

WATU 10 wanaodaiwa kuwa wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wanashilikiwa na polisi mkoa wa kipolisi wa Tarime Rorya mkoani Mara kwa tuhuma za kupanga mipango ya kufanya uhalifu kwenye kampeni za uchaguzi.

Kamanda wa Polisi Tarime Rorya, Kamishna Msaidizi (ACP) William Mkonda, amethibitisha kukamatwa kwa watu hao ambao alisema walikuwa ndani ya nyumba moja katika mji wa Sirari mpakani mwa Tanzania na Kenya.

"Tumewakamata watu 10 wanaodaiwa wafuasi wa CHADEMA usiku wa kuamkia Oktoba 6, mwaka huu, wakiwa katika mipango ya kufanya uhalifu katika kampeni zinazoendelea kati ya hao wamo wa mikoa mbalimbali wakiwamo kutoka Zanzibar.

"Tunaendelea kuwahoji ili kujua kwa undani zaidi kuhusu kuwapo kwenye nyumba moja usiku na taarifa zingine tutatoa baadaye," alisema.

Mkonda aliwataja wahutumiwa wanaohojiwa kuwa ni Abdallah Khalfan, Nehemia Mkama, Ramadhan Talai, Victor Fuko, Rofi Shango, Paulo Marisha, Nicolaus Manko na Zephania Sitembela, Yusuf Chibonda na Marwa Mwibari.

Mbali na watuhumiwa hao, alisema wanaendelea na msako wa watu wengine wanaodaiwa kuhusika katika vitendo vya uhalifu na uvunjivu wa amani katika wilaya za Tarime na Rorya. Mwishoni mwa wiki iliyopita, watu wanaodaiwa kuwa wafuasi wa CHADEMA, waliwavamia wenyeviti wawili wa vitongoji kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Chacha Tasha wa Buriba aliyekatwa mapanga shavuni na sikioni na Julius Mwita wa Bondeni aliyekatwa mapanga kichwani na kupigwa nondo.

Sambamba na wenyeviti hao, wanachama wengine wa CCM, Manga Antony, alikatwa kichwani na kupigwa nondo na Godfrey Sirima alikatwa kichwani na kupigwa nondo na hali yake ni mbaya.

Shirima anatarajiwa kusafirishwa kwenda Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando, Mwanza.

Tukio la kuvamiwa na kujeruhiwa kwa watu hao, lilitokea mchana wakati wakienda kwenye mkutano wa mgombea udiwani kupitia CCM, Amos Sagara, aliyekuwa na mkutano kijiji cha Buriba.



Mgombea wa urais kwa tiketi ya Chama cha ADC, Queen Cuthbert Sendiga, akihutubia mkutano wa kampeni katika kijiji cha Kichonda, Wilaya ya Liwale mkoani Lindi juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgombea urais SAU ajinadi kwa amani

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MGOMBEA urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia SAU, Muttamega Mgaywa, amesema kama atachaguliwa kuwa Rais wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, atakuwa mstari wa mbele kulinda amani iliyopo.

Alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani Morogoro baada ya kushindwa kufanya mkutano wa kampeni kutokana na kuchelewa kufika mkoani humo.

Alisema pamoja na kwamba suala la kulinda amani ya nchi ni jukumu la Watanzania wote, lakini baada ya kuapishwa kuongoza taifa, atahakikisha nchi haiingii katika vita ya aina yoyote.

Mgaywa kadhalika aliwaomba wananchi kumchagua ili aweze kufanikisha sera za chama chake ikiwamo kumwezesha kila Mtanzania shilingi milioni moja.

Aliongeza kuwa sera nyingine zenye lengo la kuwapa raha Watanzania ni elimu na afya bure kwa watu wote, na kutoa posho ya kuishi yatima, walemavu na wazee sambamba na kujenga mabweni ya wanafunzi kwa shule zote za sekondari za serikali.

Alisema sera za chama chake zinatekelezeka kutokana na utajiri wa Tanzania hasa kwenye sekta ya madini, utalii na viwanda ambavyo kwa kiasi kikubwa vimechangia nchi kuingia katika uchumi wa kati.

"Nataka niwahakikishie Watanzania kwamba sera za SAU zinatekelezeka kutokana na utajiri tulionao, tunaposema elimu bure kuanzia awali hadi chuo kikuu, pamoja na kuwezesha kila Mtanzania shilingi milioni moja, serikali yangu itajenga nyumba za kuishi milioni moja ambazo wananchi watapewa na kulipa kidogo kidogo," alisema Mgaywa.

## RC aonya watakaovuruga uchaguzi

**Alphonce Kabilondo,** GEITA

SERIKALI imesema haitasita kuwachukulia hatua watu au makundi yaliyojipanga kuvuruga uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Luhumbi, alisema hayo jana katika kikao baina ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na wawakilishi kutoka makundi mbalimbali ya vijana, wenye ulemavu, wanawake, wazee na viongozi wa dini mjini hapa.

Luhumbi, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, alisema serikali mkoani hapa imejipanga kikamilifu kuhakikisha uchaguzi huo unafanyika na kumalizika kwa amani, hivyo kuonya watu au makundi yaliyojipanga kuacha mara moja kutojihusisha na kuvuruga uchaguzi.

"Ziko taarifa za kiintelijensia kuwa kuna makundi yamejipanga kuvuruga uchaguzi mkuu kwa kuwatisha wanawake, wazee na wenye ulemavu. Nawaonya kutojihusisha na mchezo huo, kwani tutawashughulikia ipasavyo," alisema.

Mkurugenzi Msaidizi wa Mipango wa NEC, Adam Mkina, aliwataka wagombea nafasi za uongozi katika uchaguzi huo, kupitia vyeo vyao, kuzingatia kanuni taratibu na sheria za uchaguzi pamoja na sheria za nchi katika kipindi hiki cha kampeni.

Alisema baadhi ya wagombea wamekuwa wakitumia mianya ya kampeni kuvunja sheria wakidhani sheria za nchi zimesimama, hivyo kusisitiza kuwa, watashughulikiwa ipasavyo.

Pia alisema maandalizi ya uchaguzi yameshakamilika na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi pamoja na waratibu wa mikoa wameshapata mafunzo.

Mkina alisema wapigakura 29,188,347 wameandikishwa katika daftari la wapigakura, wanawake wakiwa 14,691,743 sawa na asilimia 50.33 na wanaume 14,496,604, ambao ni sawa na asilimia 49.67, huku watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali wakiwa asilimia 13.211.

Naye Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Geita Mjini, Modest Apolinary, aliwataka wananchi kutokubali kurubuniwa na kuuza kadi za kupigia kura kwa kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria.

## HABARI KITAIFA

# Chuo Mwalimu Nyerere chajivunia mafanikio

**Na Romana Mallya**

CHUO cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA) kilichoko Kigamboni jijini Dar es Salaam, kimepata mafanikio kadhaa ndani ya miaka mitano ikiwamo kuongeza idadi ya udahili wa wanafunzi kwa asilimia 19.5 kutoka wanafunzi 1,570 mwaka 2015 hadi 8,043 mwaka huu.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Shadrack Mwakalila, alieleza hayo jana baada ya kukutana na wahariri na waandishi wa habari wa vyombo tofauti ili kueleza mafanikio kwa kipindi hicho.

Alisema ongezeko hilo la wanafunzi ni katika kampasi ya Kivukoni jijini Dar es Saalam.

"Katika kampasi ya Karume Visiwani Zanzibar udahili umeongezeka kutoka wanafunzi 22 mwaka 2015 hadi 1,753 mwaka 2019. Kwa ujumla idadi imeongezeka kutoka wanafunzi 1,592 mwaka 2014/15 hadi wanafunzi 9,799 mwaka 2019/20," alisema. Alisema wameongeza idadi ya wahitimu katika kampasi ya Kivukoni kutoka 569 katika mwaka wa masomo 2014/15 hadi kufikia 3,237 kwa mwaka wa masomo 2018/19.

Prof. Mwakalila alisema wameboresha mitaala yote ikiwamo kuingiza somo la uongozi, maadili na uzalendo katika mitaala yote, ili kila mwanafunzi awe na ufahamu na kutosha kuhusiana na eneo hilo.

Mafanikio mengine, aliyataja ni idadi ya wahadhiri wenye Shahada ya Uzamivu (PhD) imeongezeka kutoka wawili mwaka 2015 hadi 35 mwaka 2020.

"Tumeongeza idadi ya programu ya mafunzo ya kitaaluma kutoka propramu tatu za shahada zilizokuwapo mwaka 2015 hadi kufikia programu 10 za shahada na programu moja ya umahili mwaka 2020," alisema.

Alisema kwa sasa chuo kina programu 10 ngazi ya shahada, 11 ngazi ya stashahada na programu 11 ngazi ya astashahada.

"Tumeongeza idadi ya vitabu zaidi ya 20,000 katika maktaba za chuo kwenye kampasi ya Kivukoni, Karume na Pemba," alisema.

Pia alisema wametoa mafunzo ya muda mfupi ya uongozi, maadili, utawala bora na uzalendo kwa watendaji serikalini pamoja na wahitimu wa chuo zaidi ya 3,000.

Pia chuo kimemalizia ujenzi wa hosteli ya wanafunzi uliosimama tangu mwaka 2014 kwa sababu ya ukosefu wa fedha na ina uwezo wa kuchukua watu 720.

Kadhalika, alisema wamekamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 300 kwa pamoja ambao ndani yake una ofisi 10 za wafanyakazi.

Prof. Mwakalila alisema wamepeleka zaidi ya wahadhiri 40 kwenye mafunzo ya Shahada ya Uzamivu katika fani mbalimbali za kitaaluma.

Alisema wametoa bunifu 22 kwa mwaka wa masomo 2019/20 na wanafunzi watano walishiriki mashindano ya kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) na Muhamed Ramadhan alishika nafasi ya pili kwa kubuni mfumo wa kutambua na kudhibiti upotevu wa gesi katika mitungi.

Prof. Mwakalila alisema wametenga bajeti na kuanza mchakato wa ujenzi wa hosteli katika kampasi ya Karume visiwani Zanzibar ambayo ikikamilika itachukua wanafunzi 1,536.

Pia alisema wametenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa maktaba katika kampasi ya Kivukoni, Dar es Salaam itakayokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500.

Alisema wamefungua kampasi ya Pemba, na kwamba wanatarajia kujenga chuo kingine Dodoma, ili kujitanua na kusogeza huduma maeneo mengine nchini.


**BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**NOTISI NA TANGAZO LA MDANA**

Kwa Idhini tuliyopewa na ***BANK OF AFRICA (BOA)*** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo huo kwa **MNADA WA HADHARA.** Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO |
|---|---|---|
| 1. | RAMADHANI MASOUD | Nyumba ya makazi yenye hati na.62514 PLOT na.66, BLOCK 3 bweni Mpiji. Dar es salaam kwa jina la RAMADHANI MASOUD |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**Bank of Africa**
**Head Office,**
**NDC Development House, ohio street-kivukoni**
**P.O. BOX 3054,**
**DAR ES SALAAM**
**Tel: +255-22-2110104/2111290**
**Fax: +255-22-2113740**

215933602


# Majaliwa ataka uhakiki kampuni ya mbolea

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa (pichani), ametoa siku tatu kwa Wizara ya Kilimo kukutana na menejenti ya kampuni ya utengenezaji na usambazaji wa mbolea ya YARA ili kuhakiki na kupata ithibati ya mbolea ya bure itakayogawiwa kwa wakulima wadogo kupitia mpango wa Action Africa.

Majaliwa alitoa agizo hilo jana alipotembelea kiwanda cha YARA kilichoko jijini Dar es Salaam na kuipongeza kampuni hiyo kwa uwekezaji mkubwa na utekelezaji wa mpango huo wenye thamani ya Sh. bilioni 16.5.

"Serikali inawashukuru sana YARA kwa kutoa mbolea kwa ajili ya wakulima nchini. Lakini ni muhimu ithibati ifanyike ili iruhusu mbolea iende kwa wakulima. Mpango huu ni mzuri kwa sababu unaendana na malengo ya serikali katika kukuza sekta ya kilimo hasa uzalishaji wa chakula," alisema.



Waziri Mkuu alisema serikali ina nia njema ya kuunga mkono wadau wanaosaidia sekta ya kilimo na kuwahakikishia wawekezaji hao usalama na mazingira mazuri ya uwekezaji hapa nchini.

Pia Waziri Mkuu alitoa wito kwa kampuni na taasisi zingine kuiga mpango huo wa YARA.

Majaliwa alimwomba Balozi wa Norway nchini, Elizabeth Jacobsen, kuanzisha Jukwaa la Biashara kwa wafanyabiashara wa Tanzania na Norway ili wapate uzoefu wa kibiashara kutoka kila upande.

Mkurugenzi Mtendaji wa YARA, Winston Odhiambo, alisema mpango huo utawanufaisha wakulima wadogo 83,000 nchi nzima, ambapo tani 12,500 za mbolea zitagawiwa bure kwa wakulima wa mahindi na mpunga.

Odhiambo alisema kuwa mpango huo una lengo la kusaidia uzalishaji wa chakula ambapo wanufaika pia watapewa ushauri wa bure kutoka kwa mabwana shamba wa kampuni ya YARA ili kuleta ufanisi katika uzalishaji.

Naye Balozi Jacobsen alisema mpango huo ni sehemu ya utekelezaji wa malengo ya dunia kuhusu uhakika wa upatikanqji wa chakula katika Bara la Afrika.

Wanufaika wa mpango huu ni wakulima wadogo kwa ajili ya msimu huu wa kilimo ulioanza Septemba hadi Desemba, mwaka huu, ambao tayari wamekwishasajiliwa kupitia mpango huo.


**BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na ***NMB BANK PLC*** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo huo kwa **MNADA WA HADHARA.** Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE | TAWI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ZAHARA HUSSEIN | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye Kiwanja chenye **Leseni** ya makazi maeneo ya **Mangaya Mbagala TMK/MBGL/MAN11/269A** Manispaa ya **Temeke** | 07/11/2020 | MBAGALA |
| 2. | FRANCIS ALEX MASSAWE | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye Kiwanja chenye **Hati** ya mauziano maeneo ya **Bunju "A"** Manispaa ya **Kinondoni** iliyopo kwa jina la **Moshy Mohamed Malinda** | 30/10/2020 | ILALA |
| 3. | MANENO LUMAN ANTHONY | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye **Kiwanja** chenye **Hati** ya mauziano maeneo ya **Kinyerezi** Manispaa ya **Ilala** | 23/10/2020 | ILALA |
| 4. | AYUBU JOHNAS KIYOMBO / SEZARY DONASIAN MASANSA | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye **Kiwanja** chenye **Hati** ya Mauziano maeneo ya **Mivumoni** Manispaa ya **Kinondoni** iliyopo kwa Jina la **Sezari Donasian Masansa.** | 30/10/2020 | ILALA |
| 5. | SPECIAL AFRICA / CONSOLATA SAMIRA | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye **Kiwanja** chenye **Hati** ya Mauziano maeneo ya **Malamba Mawili** Manispaa ya **Ubungo.** | 23/10/2020 | ILALA |
| 6. | TULLO YOHANA HEMBA | Nyumba ya Makazi iliyopo mtaa wa kwenye **Kiwanja** chenye **Hati** ya Mauziano maeneo ya **Ilala** iliyopo kwa Jina la **Tullo Yohana Hemba.** | 07/11/2020 | ILALA |
| 7 | MURO GENOVEVA NDENUMBI | Nyumba ambayo haijakamilika iliopo kwenye kiwanja chenye Hati ya mauziano maeneo ya Kimara Temboni inayosomeka kwa jina la **Genoveva Ndenumbi** Manispaa ya **Ubungo.** | 23/10/2020 | KKOO |
| 8 | MKENDO HOME APPLIANCE | Nyumba ya makazi iliopo kwenye kiwanja chenye hati ya mauziano maeneo ya Kifuru inayosomeka kwa jina la **Fadhili Shabani Magembe** manispaa ya Ilala | 30/10/2020 | ILALA |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**NMB Bank PLC,**
**Ohio Street / Ali Hassan Mwinyi Road,**
**P.O. BOX 9213,**
**DAR ES SALAAM**
**Telephone: +255 22 2322550**
**email: Benedicto.Baragomwa@nmbbank.co.tz**

115933502

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Zimebaki siku 20, tutembelee vituo vya kupigia kura

**ZIMEBAKI** siku 20 Watanzania waliojiandikisha kupiga kura katika daftari la kudumu la wapiga kura, kufanya uamuzi ndani ya sanduku juu ya diwani, mbunge na rais wa kuwaongoza kwa miaka mitano.

Ndani ya kipindi hiki wagombea vinazunguka huku na kule kushawishi wananchi wawachague ili waongoze.

Maboresho ya daftari la kudumu la wapiga kura yalishafanyika mwaka 2019 na mwaka huu, na baada ya hapo daftari la awali liliwekwa wazi katika vituo mbalimbali kwa ajili ya wananchi kuangalia majina yao kama yako sahihi kabla ya kutengenezwa kwa daftari la mwisho.

Aidha, maboresho hayo yalihusu kuondoa majina ya waliofariki, kuingiza majina ya waliofikisha umri wa miaka 18 na kubadili taarifa za waliohama maeneo.

Wapo aliohama maeneo lakini hawakurudi kubadili taarifa zao maana yake ni kuwa siku ya kupiga kura ni lazima warudi katika maeneo yao ya waliojiandikisha kwa ajili ya kupata haki ya kuchagua viongozi wanaoona wanafaa.

Ni muhimu sana kila Mtanzania akafika kwenye kituo alichojiandikishia kuangalia kama jina lake lipo, hiyo ni kujihakikishia kuwa Oktoba 28, mwaka huu, atakuwa ni miongoni mwa Watanzania waliotekeleza wajibu wa kikatiba.

Kwa mujibu wa taarifa iliyopo kwenye tovuti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), katika uchaguzi huu kutakuwa na jumla ya vituo vya kupigia kura 80,155 , waliojiandikisha kupiga kura ni Watanzania 29,188,347 kwa ajili ya kuchagua rais, wabunge wa majimbo 390 na madiwani wa kata 5,350.

Wagombea wanaopigiwa kura ni kutoka vyama vya 19 vyenye usajili wa kudumu kutoka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, na ambao wamesimamisha wagombea katika nafasi hizo.

Matarajio ya Watanzania wengi ni kuhakikisha NEC inaweka wazi daftari ikiwamo kuhakikisha kila chama kinapata, ili kila mmoja ajiridhishe ikiwa ni namna ya kuhakikisha uwapo wa uchaguzi huru na haki.

Katika mchakato wa uchaguzi mbali na wagombea kufanya kampeni, lakini bado kuna taasisi zaidi ya 90 zimepewa kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura kwa wananchi.

Tunaamini ziliwafikia wapigakura hasa wa maeneo ya vijijini ambao ni wahitaji zaidi ya waliopo mjini.

Waliopo mjini wanafikiwa vyombo vya habari, mitandao kwa urahisi zaidi ikilinganishwa na maeneo ya vijijini ambayo wakati mwingine kuna changamoto ya mitandao ya kuwawezesha watu kuingia kwenye mitandao na kupata habari mbalimbali.

Lakini pia ni wachache wanaofikiwa na magazeti ni wachache ili wapate elimu husika, na ndiyo maana taasisi hizo zilipewa kibali cha kufanya ziara maeneo mbalimbali nchini kuwafikia wananchi kokote waliko.

Kila mmoja ana wajibu wa kufanikisha uchaguzi mkuu, na kila mgombea ana wajibu wa kuhakikisha uchaguzi huu unakuwa wa amani.

Na zaidi vyombo vya dola na mamlaka nyingine za serikali zinapaswa kutenda haki sawa kwa wagombea wote, na si kuonyesha ubaguzi ambao huenda ukasababisha wengine kujiona hawastahili ndani ya ardhi yao kwa jambo ambalo ni la kikatiba.


Inapotokea vyombo vya dola vinalaumiwa au kuhusika katika kuumiza upande wowote ni rahisi kuwapo kwa malalamiko mengi ambayo yatatia dosari uchaguzi.

Tayari mataifa mbalimbali duniani yameelekeza macho na masikio yao kwenye uchaguzi huu kwa kusisitiza haki na uhuru kuonekana upo na umetendeka katika uchaguzi mkuu.


Haitarajiwi kuona mawakala wa vyama wakizuiwa kuapishwa, kuingia na kupewa nakala za matokeo ya kura, bali usawa na haki ikitawala uchaguzi utaliingiza taifa katika rekodi mpya za haki, amani na usawa kwa watu wote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Shule inapowanoa wanafunzi kuvuna nje ya mitaala ilipo

Na Yasmine Ptotace, Mkuranga

**KUNA** usemi au msaimati 'mkakati.' Msingi wake ni kitu kinachoandaliwa katika mfumo mara nyingi wa maandishi, ukilenga kusimamia sera, ikiwa ni kwa ajili ya jambo fulani, kwa walengwa mahsusi.

Ili kuifanya ilete mabadiliko katika sehemu, mikakati hupangwa kwenye maeneo mbalimbali, katika mtazamo wa kutimiza lengo husika.

Hivi karibuni, uongozi wa Shule ya Saint Mathew iliyopo Kongowe wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani, ulieleza namna shule ilivyoweka mikakati ya miaka 10 ijayo kuongeza stadi ya utoaji elimu bora.

Anautaja mkakati huo ni pamoja na kuwafundisha watoto stadi za maisha, ukiwamo ujuzi unaowasaidia wanafunzi ufahamu sahihi kuhusiana na uhalisia wa ujasiriamali ulikosimamia, ili hata unapofika wakati wanahitimu masomo yao, wote shuleni wawe na uwezo wa kujiajiri.

Ni maelezo yalioyobeba sura ya uongozi na zao lake la mafunzo, ikiaminika itakuwa mkombozi kwa wanafunzi kujiamini katika kuhangaikia maisha na kuweka kanda lugha potofu ya kupenda kukaa vijiweni.

Anaongeza kuwa, mikakati mwingine uliopo katika shule yao, ni pamoja na wanafunzi kufundisha kutengeneza kamera za usalama aina ya CCTV.

Ni mkakati unaojitafsiri kwamba, mwaka ujao shule hiyo itaanza kuwafundisha wanafunzi masomo ya kupika na kushona, lengo hilo ni kumsaidia mtoto kujisajili kimaisha na akaacha falsafa ya kukaa vijiweni, ambayo shule kwa ujumla wake unaipinga vikali.

Hadi sasa shuleni Saint Mathew, wanafunzi vijana wanafundishwa maadili na malezi, huku matunda yakijianika kwamba hakuna mtoto aliyewahi kuacha masomo kutokana na kupata ujauzito.

> **Ni mkakati unaojitafsiri kwamba, mwaka ujao shule hiyo itaanza kuwafundisha wanafunzi masomo ya kupika na kushona, lengo hilo ni kumsaidia mtoto kujisajili kimaisha na akaacha falsafa ya kukaa vijiweni, ambayo shule kwa ujumla wake unaipinga vikali.**

Inaelezwa kwamba, kutokana na maadili ambayo wanafunzi wameyapata, yamewasaidia kwa kiasi kikubwa kubadilika na kuwa mfano wa kuigwa kutokana na kufanya vizuri katika masomo yao.

Ni mabadiliko yanayotajwa shuleni hapo kwamba yamewasaidia wanafunzi kufanya vizuri kwenye mitihani yao ya mwisho shuleni, hata kupata asilimia ya ufaulu inayotajwa kwa msamiati '98'.

Anaongeza kuwa shule yao haibagui wanafunzi, inacukua wanafunzi wa namna zote, pasipo kujali uwezo wao kitaaluma, shule inafanya kazi ya kuwasaidia na hatimaye wamekuwa wakishuhudiua matunda bora ndami ya ulingo wa taaluma.

Uongozi wa shule unakiri kufahamu kuwapo baadhi ya shule ambazo hazichukui wanafunzi wenye uwezo duni kitaaluma, hali inayowanyima haki baadhi ya watoto,

Inaelezwa kwa sasa, shule ya Saint Mathew kwa kuliona hilo, inachukua jukumu la kuwasaidia watoto walio chini kimasomo, wakiwakweza kwa mbinu za kitaaluma, nao wanakwea kwa ubora kileleni.

Pia, mbinu nyingine inayotumika, inatajwa ni kuafuata na kuwashauri wazazi wasibweteke na kukimbilia kwenye viwango vya ufaulu pekee, pia wageuze hisia kwa kipengele muhimu zaidi ambacho ni kuangalia maadili.

Anasema mkakati mwingine ulioko ni mwakani shule itaanza kufundusha lugha ya Kichina na hadi sasa kuna wanafunzi 17 waliopelekwa kujifunza lugha hiyo.

HABARI KITAIFA

# NEC yaahidi uchaguzi utakuwa huru na haki

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesisitiza kuwa itaendesha uchaguzi wenye ushindani wa haki kwa wagombea wote, huku ikitangaza asasi za kiraia 113 za ndani na nje ya nchi kupewa vibali rasmi vya kuwa watazamaji.

NEC imesema kati ya asasi hizo, 97 zinatoka ndani ya nchi na 16 nje ya Tanzania ambazo zitapata fursa ya kufuatilia uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari na wadau wengine wa uchaguzi, Kamishna wa NEC, Jaji mstaafu Thomas Mihayo, alisema mwaka huu uchaguzi utaendeshwa kwa haki, kuzingatia sheria, katiba na ushindani ulio sawa kwa wagombea wote.

Jaji Mihayo alivitaka vyama vyote vya siasa, wagombea na wananchi, kuepuka kutumia lugha za kashfa na maneno ya uchochezi yanayotishia usalama na amani ya nchi katika kipindi hiki cha kampeni.

"Tutahakikisha wagombea wanaepuka kufanya kampeni ambazo zinaashiria ubaguzi katika misingi ya jinsia, ulemavu, ukabila, udini, maumbile au rangi," alisema.

Kuhusu vifaa muhimu kwa ajili ya uchaguzi huo, Jaji Mihayo alisema vimeshapatikana pamoja na utoaji wa elimu kwa wapigakura na waratibu wa uchaguzi.

Alisema mafunzo muhimu yaliyobaki ni yale yanayowahusu watendaji wa vituo ambayo hufanyika siku chake kabla ya uchaguzi.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Luphingo Mwasalujonja, alisema wapigakura 29.5 wanatarajia kupiga kura katika uchaguzi mkuu ujao.

Alisema katika maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu, NEC haikugawa majimbo ya uchaguzi bali ilibadilisha majina ya majimbo yaliyoko katika Wilaya ya Chamwino na kuifanya Chilonwa kuwa Chamwino na Mtera kuwa Mvumi.

"Tume itatumia vituo vya kupigia kura 80,155 na kati ya hivyo, Tanzania Bara itakuwa na vituo 79,670 na Tanzania Zanzibar itakuwa na vituo 485," alisema.

Aliongeza kuwa ili kurahisisha shughuli za upigaji kura, kila kituo kitakuwa na wapigakura wasiozidi 500.

# Mradi miundombinu Dar wafikia 80%

**Na Mary Geofrey**

MRATIBU Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP), Humphrey Kanyenye, amesema ujenzi wa miradi ya barabara, vituo vya mabasi, masoko, mifereji ya majitaka na ujenzi wa vyoo imekamilika kwa asilimia 80.

Amesema miradi hiyo iliyofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 660, awamu ya kwanza ilianza mwaka 2015 na inatarajiwa kukamilika mwakani.

Kanyenye alielezea maendeleo ya mradi huo jana, jijini Dar es Salaam, katika ziara ya uongozi wa Bodi ya DMDP ya kutembelea miradi hiyo katika Manispaa ya Temeke, ambako walikagua ujenzi wa masoko, barabara ya Kijichi, Mbagala na Mwanamtoti na Bonde la Mto Kizinga.

Alisema licha ya kasi ya ukamilishaji wanayoenda nayo bado wanakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwamo msongamano kutokana na ongezeko la watu katika mitaa na hali ya hewa wakati wa mvua.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mradi wa DMDP Temeke, Edward Simon, alisema imegawanyika katika mafungu 15 ikiwamo ujenzi wa barabara ya Kijichi-Toangoma, Mwanamtoti na ofisi ya mradi.

Alisema pia ujenzi wa barabara za Chang'ombe, Nchicha na Temeke Mbagala, ujenzi wa Bonde la Gerezani, maboresho ya bonde la Mto Kizinga na maboresho ya miundombonu ya jamii kata ya Kilakala na Keko.

"Katika awamu ya kwanza ya mradi, halmashauri inatarajia kupokea Sh. bilioni 265 na halmashauri imechangia Sh. bilioni 20.3 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa miundombinu hadi Julai mwaka huu.

"Halmashauri imepokea jumla ya Sh. bilioni 148 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika maeneo hayo," alisema Simon.

Alisema baada ya ujenzi wa miradi hiyo wamefanikiwa kupunguza foleni za magari barabarani, kupunguza kwa mafuriko ya maji vipindi vya mvua, kuongezeka kwa usalama katika jamii baada ya barabara zilizojengwa kufungwa taa, kuongeza ajira na vyanzo vipya vya mapato katika manispaa hiyo.

BIASHARA ZOTE MAKINI
HUTANGAZWA HAPA
Nipashe | Nipashe mwendo mdundo

Unafahamu ni kwa nini?
"Tunaongoza na Kuaminika"




Nipashe MWANGA WA JAMII
WASILIANA NASI
0745 700 710 au 0677 020 701
advertise@guardian.co.tz (Matangazo)
subscription@guardian.co.tz (Magazeti)
epaper@guardian.co.tz (epaper)

PATA NAKALA YAKO
https://epaper.ippmedia.com
Pakua The Guardian-IPP Media
Download on the App Store | Get it on Google Play

KUWA WA KWANZA KUHABARIKA
TUFUATE nipashetz | nipashe | TheGuardiantz | YouTube TheGuardiantz

# Zimamoto yataka taarifa za majanga kwa wakati

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

MKUU wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Kamishna Jenerali John Masunga, amewataka wananchi kuonyesha ushirikiano kwa jeshi hilo kwa kutoa taarifa mapema yanapotokea matukio ya moto.

Masunga alitoa rai hiyo, alipotembelea ofisi za jeshi hilo mkoani Iringa, ili kuangalia utendaji wa kazi.

Kamishna Masunga alisema taarifa za matukio ya moto zinaweza kutolewa kwa kupiga simu namba 114, linapotokea tatizo.

Alisema kumekuwapo na changamoto kwa mitaa kutopitika kirahisi yanapotokea majanga ya moto, hivyo kuwapa wakati mgumu katika kuzima moto na aliwaomba wataalamu wa mipango miji kuhakikisha wanatengeneza mazingira rafiki, ambayo yatalifanya jeshi hilo kufika kirahisi kwenye matukio ya moto.

Aidha, alisema serikali inatarajia kupokea magari mapya zaidi ya 30 na kwamba yatapelekwa mikoa mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha mikoa inaondokana na changamoto ya kutumia magari chakavu.

Hivi karibuni, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani hapa, lilitoa elimu kwa wananchi ikiwamo kupitia vyombo vya habari, kuhakikisha wanakuwa makini katika kukabiliana na majanga ya moto.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Exim Tanzania, Jafari Matundu (kulia), akizungumza na mmoja wa wateja wa benki hiyo, Bakari Mikidadi (aliyekaa), alipotembelea tawi la benki hiyo la Exim Tower jijini Dar es Salaam jana, ili kupata mrejesho wa huduma zinazotolewa kwa wateja ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya huduma kwa wateja. Wengine ni Meneja wa benki hiyo tawi hilo, Vishal Ratansinh (katikati) na Meneja Msaidizi Huduma kwa wateja, Rukia Chambuso. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBS yakutanisha wadau wa takwimu

**Na Elizabeth Zaya**

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS), imekutanisha wadau kutoka taasisi za umma na binafsi kwa ajili ya kujadili mbinu na kanuni za kutumia vyanzo mbadala vya kitakwimu maarufu kama 'Big Data' katika uandaaji wa takwimu rasmi.

Imeelezwa kuwa, lengo ni kusaidia utekelezaji wa mipango ya maendeleo kwa nchi.

Akizungumza wakati wa mkutano wa wadau hao jijini Dar es Salaam jana, Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema kwa sasa ofisi hiyo inawekeza zaidi nguvu zake katika kuboresha uzalishaji wa takwimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Alisema lengo la kutumia takwimu hizo ni kusaidia nchi namna ya kupanga maendeleo yake na kufuatilia viashiria vya ajenda maendeleo endelevu (SDGs), pamoja na mipango mingine ya maendeleo katika nchi.

Dk. Chuwa alisema semina hiyo ya siku mbili, ambayo iliandaliwa na NBS kwa msaada kutoka Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), inalenga kujadili na kuhakikisha inapatikana mikakati, njia bora na sahihi inayolenga kuimarisha utengenezaji wa data rasmi za maendeleo endelevu.

Pia alisema, ililenga kutambua maeneo ya ushirikiano kati ya watoa takwimu, wazalishaji na watumiaji pamoja na kukuza na kujadiliana namna bora kupata takwimu kwa ajili ya kusaidia ufuatiliaji wa maendeleo ya kitaifa, kikanda na kidunia.

Alisema NBS imejipanga kuendelea kuingiza mifumo yake ya ukusanyaji wa takwimu rasmi kwa kutumia teknolojia za kisasa, ili kuhakikisha kwamba zinakuwa ni za uhakika.

Aliwataka wadau hao kuhimiza matumizi sahihi ya takwimu katika ngazi zote za jamii katika mipango yao ya maendeleo.

Meneja wa Sayansi ya Takwimu kutoka Tanzania Data Lab, Charles Bundu, alisema ushirikiano kati yao na NBS, umekuja wakati mwafaka ambao nchi inahitaji takwimu sahihi katika shughuli za maendeleo.

Mkurugenzi wa Mipango wa UNDP, Amon Manyama, alisema wataendelea kuiunga mkono NBS hususani kwa kuwajengea uwezo, ili kuboresha uzalishaji wa takwimu rasmi na kuwezesha kufikia katika malengo makubwa zaidi waliyokusudia.

# Exim yaahidi ufanisi huduma kidigitali

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim imeahidi kuboresha zaidi huduma zake hususani za kidigitali.

Ahadi hiyo imetolewa wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Kimataifa ya Huduma kwa Wateja.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu, akiwa ameambatana na maofisa waandamizi wa benki hiyo waliotembelea matawi kadhaa pamoja na baadhi ya wateja wa benki hiyo jijini Dar es Salaam, ili kuzungumza na wafanyakazi pamoja na kupata mrejesho kutoka kwa wateja wa kuhusu huduma zinazotolewa na wateja wa benki hiyo.

"Kama taasisi inayotoa huduma muhimu kwa wateja, wiki hii ni muhimu kwetu kwa kuwa inatupa fursa ya kushirikiana kikamilifu na wateja wetu. Uhusiano mzuri na madhubuti na wateja wetu unabaki kuwa muhimu sana kimkakati na hatua hii inaonyesha nia yetu ya kutambua jambo hili," alisema Matundu alipotembelea tawi la Makao Makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam jana.

Akizungumzia umuhimu wa utoaji wa huduma kwa ubora, Matundu aliwapongeza wafanyakazi wa benki hiyo, huku akieleza kutambua namna wanavyojituma kuwahudumia wateja kwa weledi na kwa uaminifu mkubwa.

"Kila wakati tumekuwa tukitafuta njia mpya za kuwahudumia wateja wa benki ya Exim kwa weledi zaidi, huku pia tukihamasisha ukuaji wa pamoja kati yetu na wateja wetu," alisema.

Meneja Mwandamizi wa Huduma kwa Wateja wa benki hiyo, Frank Matoro, alifafanua namna benki hiyo inavyojitoa katika kuwahakikishia utoaji wa huduma bora wateja wake ili kukidhi mahitaji na matarajio yao wakati wote.

"Ni muhimu kuonyesha na kuthamini thamani ya utoaji bora wa huduma kulingana na uzoefu na mahitaji ya wateja wetu, kwa kuwa vitu hivi ni viungo muhimu katika kujenga taasisi ya kifedha yenye nguvu zaidi nchini," alisema.

HABARI KITAIFA




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (katikati), na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Bernard Konga wakibadilishana mkataba wa uzinduzi wa mpango wa "DUNDULIZA" kwa huduma za NHIF kupitia benki hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi wa benki hiyo, Filbert Mponzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mhede ataka mifumo rahisi ya kibenki

**Na Beatrice Moses,** TUDARCo

MENEJIMENTI na wafanyakazi wa Benki ya NMB wametakiwa kuendelea kubuni mifumo rahisi kwa ushirikiano na wadau wa sekta ya kifedha, ili kuongeza tija na ufanisi katika benki yetu.

Wito huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Bodi ya benki hiyo, Dk. Edwin Mhede, juzi wakati akizindua rasmi Wiki ya Huduma kwa Wateja wa NMB, ikiwa ni hatua ya kuelekea kwenye maadhimisho wiki ya wateja duniani.

"Napenda niweke wazi lengo letu kwa jamii ya Watanzania na wateja wa benki yetu ni kuongeza wateja wanaoridhishwa kwa kiwango cha juu na huduma zetu za kibenki, hivyo kuongeza idadi ya wateja wanaotumia huduma za Benki ya NMB," alisema.

Dk. Mhede ambaye ni Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), alisema NMB imefanikiwa kuzindua huduma tatu za kidigitali, ambazo zinalenga kuboresha huduma kwa wateja.

"Huduma hizi naomba zilete chachu katika mtazamo wa jinsi tunavyotoa huduma kwa wateja, ili tuweze kubuni zaidi njia mbadala za kuongeza tija katika eneo hili," alisema.

Awali Oktoba 5 mwaka huu benki hiyo ilifanikiwa kuzindua huduma tatu za kidijitali zinazokusudia kuboresha na kukidhi matarajio ya wateja huku zikiongeza ukaribu kati ya benki na wateja wake.

Huduma hizi zilitajwa kuwa ni za kituo cha huduma kwa wateja kupitia mtandao wa WhatsApp kwa kutumia namba: +255 747 333 444, pili ni huduma ya kurejesha tokeni ya LUKU kwa kupiga namba ya bure 0800 002 002 na ya tatu njia mbadala na ya haraka ya kupokea maoni ya wateja papo kwa papo kupitia "Quick Response" au QR code. Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, alisema wamejipanga vyema kutumia teknolojia kuboresha huduma kwa ajili ya wateja wao.

"Nina furaha kuzindua huduma hizi za kidijitali, ambazo zitakidhi mahitaji ya wateja wetu kwa kuwapa huduma mbadala na za kibunifu za kibenki zenye fursa ya kutoa mrejesho na maoni yao kuhusiana na huduma zetu za kibenki," alisema Zaipuna.

Aliongeza: "Katika maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja mwaka huu, tumezindua huduma hizi muafaka zitakazotuweka karibu zaidi na wateja wetu na kuleta chachu katika utoaji huduma kwenye sekta ya kibenki nchini."

# Vikwazo majarida kitaaluma vyabainishwa

**Na Vincent Mpepo,** OUT

IMEBAINIKA kuwa shughuli za uchapishaji wa majarida, matini na machapisho ya kitaaluma, ambazo ndio uti wa mgongo wa misingi ya kitaaluma zimekuwa na changamoto kiasi cha kuwakosesha baadhi ya wahusika haki zao za msingi.

Hayo yamejitokeza katika majadiliano miongoni mwa washiriki wa warsha ya siku tano kuhusu uandishi wa makala, machapisho na matini mbalimbali za kitaaluma inayoendelea katika ukumbi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT).

Akiwasilisha mada katika warsha hiyo, Prof. Mugyabuso Mulokozi alisema uchapishaji wa kazi mbalimbali za kitaaluma ni kazi ngumu ambayo inahitaji umakini na muda mwingine hata muda wa ziada, ili kuhakikisha upatikanaji kazi za kitaaluma zinazokidhi ubora.

"Kulegalega kwa shughuli za uchapishaji wa majarida ya kitaaluma katika taasisi nyingi za elimu ya juu kunatokana na changamoto za kiuendeshaji," alisema Prof. Mulokozi.

Alisema katika mchakato wa kufanikisha jambo lolote hususani uchapishaji lazima kuna gharama zinahusika, hivyo lazima masuala yote kuhusu haki za wahusika kwenye mnyororo wa uchapishaji ziangaliwe, ili kuwapa motisha ya kazi waifanyayo.

"Wahariri wa majarida ya kitaaluma wanasahaulika katika kupewa walau kifuta jasho, huku wakati mwingine ikisemwa kazi hizo ni sehemu ya majukumu yao," alisema Prof. Mulokozi.

Mshiriki wa warsha hiyo Mhadhiri Evaristo Mtitu wa Kitivo cha Elimu chuoni hapo alisema, kumekuwa na changamoto ya baadhi ya vyuo nchini kuwa na mifumo, ambayo haikubali kazi za kitaaluma kutoka taasisi nyingine za elimu ya juu hivyo kuwakosesha haki za upandaji madaraja kitaaluma.

# Kituo cha yatima chaomba kusaidiwa

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu cha Mwandaliwa kilichopo Mbweni, Kinondoni jijini Dar es Salaam, kimewaomba watu wenye nia njema kuendelea kujitolea kuwasaidia watoto wanaolelewa katika kituo hicho.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi wa Kituo hicho, Haji Bakhulla, wakati akizungumza katika ofisi za Nipashe, zilizopo Mikocheni, Dar es Salaam.

Bakhulla alisema kusaidia watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu ni miongoni mwa nia njema ya kuonyesha uzalendo na pia ni ibada kwa Mwenyezi Mungu.

"Kituo chetu mtu aliyekianzisha kwa nia njema ya kusaidia watoto hao alifariki, lakini kwa sababu tayari tulikuwa tumeshajitolea kusaidia watoto na wanaoishi katika mazingira magumu, ambao wanatoka katika familia za Watanzania wenzetu tulisema hatutakata tamaa, tuliendelea kusali na kumwomba Mungu atusaidie tusiache kutoa huduma hii," alisema Bakhull.

"Tunashukuru bado tumeendelea kupata nguvu ya kutoa huduma hii na tumesaidia watoto wengi wenye matatizo mbalimbali, na baadhi ya watu wamekuwa wakituunga mkono kufanikisha kazi hii ya kuwasaidia watoto na Watanzania wenzetu."

Alisema wanakaribisha kila Mtanzania, ambaye ataguswa kuwaunga mkono kwa msaada wa aina yoyote kwa ajili ya kusaidia kuongeza nguvu ya kutoa msaada huo kwa wenye uhitaji waliopo katika kituo hicho.

Alitoa wito kwa mtu atakayeguswa kuwaunga mkono kusaidia watoto hao, kufika katika kituoni hicho cha Mwandaliwa kilichopo Mbweni au kuwasiliana nao kupitia namba 0757 555 511.

# Watakiwa kuzingatia afya ya watoto mvua za vuli

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WAKAZI wa Mkoa wa Kagera wametakiwa kuzingatia afya ya watoto wao hasa wakati wa msimu wa mvua za vuli, ili kuwaepusha kukumbwa na magonjwa ya kuambukiza ikiwamo malaria.

Akizungumza na Nipashe, mshauri wa kitengo cha damu salama Mkoa wa Kagera, Bashweka Amos, alisema kuwa wakati wa msimu wa mvua za vuli wananchi wengi huelekeza mawazo yao katika kuandaa mashamba, huku wakisahau kuangalia afya ya watoto wao.

"Mtoto asipotunzwa na kulishwa vizuri na kwa wakati ataugua mara kwa mara, afya yake itateteleka na kumfanya awe na lishe duni, hii husababisha kuugua mara kwa mara na kupungukiwa damu," alisema.

Amos alisema kuwa katika kipindi hicho mahitaji ya damu huwa makubwa, huku akisema mahitaji ya damu yanakuwa makubwa wakati wa kiangazi, kutokana na mama wajawazito na watoto kuugua.

Akizungumzia kampeni ya wiki ya uchangiaji damu kitaifa iliyoanza Septemba 21 hadi 25, alisema kuwa Mkoa wa Kagera haukuweza kufikia lengo lililowekwa la kukusanya chupa 1,350 na badala yake walikusanya chupa za damu 577.

## Ofisa elimu ataka somo la ujasiriamali shuleni

**Na Yasmine Ptotace,** MKURANGA

OFISA Elimu (Sekondari) Mkoa wa Pwani, Hadija Ally Mchea, amewataka wanafunzi wanaohitimu kidato cha nne wasikae vijiweni, badala yake wajiajiri kupitia masomo ya ujasiriamali, waliyoyapata shuleni.

Hadija aliyasema hayo, katika mahafali ya 20 ya kidato cha nne, katika Shule ya St.Mathew's, Mkuranga mkoani Pwani.

"Nimeona mmejifunza ujasiriamali wa aina mbalimbali, sasa mnamaliza shule, masomo ya ujasiriamali muyaendeleze na sio kukaa vijiweni," alisema Mchea.

Aliongeza kuwa elimu ya ujasiriamali ambayo wameipata itawasaidia kunyanyuka kiuchumi.

Alisema Tanzania imeingia uchumi wa kati, hivyo elimu ya ujasiriamali itafikiwa, iwapo wanafunzi watayaendeleza yale wakiofundishwa.

Alisema serikali inatambua mchango unaotolewa na shule za binafsi na kuahidi kuwa serikali itaendelea kushirikiana nazo.

Mwalimu mkuu wa shule hiyo, Joseph Nalaila, anasema nidhamu iliyopo kwa watoto wao ndio imekuwa msaada katika shule, ambapo kila mwaka ufaulu unaonekana kuwa juu kila mwaka.

## NBC yaahidi weledi huduma kwa wateja

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imeahidi kuendelea kuzingatia weledi katika utoaji wa huduma zake sambamba na kuboresha zaidi ushirikiano kwa wateja wake.

Hayo yalibainishwa wakati wa uzinduzi wa mwezi wa huduma kwa wateja wake jijini Dar es Salaam.

Katika uzinduzi wa kampeni hiyo ya mwezi mmoja iliyoanza, ilishuhudiwa wafanyakazi pamoja na watendaji wakuu wa benki hiyo, wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Theobald Sabi, wakiwakaribisha kwa kuwapigia makofi ya heshima wateja wa benki hiyo waliokwenda kupata huduma kwenye tawi la Makao Makuu jijini Dar es Salaam.

"Tumetenga mwezi mzima kwa ajili ya huduma maalum kwa wateja wetu kwa kutambua na kuthamini nafasi yao muhimu katika kuifanya Benki ya NBC kuwa benki kubwa na yenye faida zaidi nchini. Hii inakuja wakati ambapo pia tumewekeza zaidi katika kuwapatia huduma nzuri na rafiki kwao,'' alisema Sabi alipokuwa akifungua kampeni hiyo.

mwezi huo wa huduma kwa wateja kama fursa nzuri ya kuboresha zaidi muonekano wake kwa mamia na maelfu ya wateja wake kote nchini.

"Mafanikio tunayojivunia leo ni kwa sababu ya wateja wetu waliotuamini wameendelea kuwa waaminifu kwa muda mrefu, ndiyo sababu tunasherehekea nao pamoja," alisema Sabi na kuongeza: "Kwa miongo kadhaa, tumeunda uhusiano mzuri na wateja wetu wanaokua haraka kimafanikio na tunaendelea kujitolea kuwapatia suluhisho za kifedha za ubunifu na zenye uwajibikaji, ambazo zinawawezesha kuendelea kukua zaidi."

Meneja wa Huduma kwa Wateja wa benki hiyo, Salama Musa, alisema katika kipindi chote cha mwezi huo shughuli kadhaa zimepangwa kwa ajili ya wateja wa ndani na nje katika kuthamini na kuimarisha zaidi mahusiano ya pande zote mbili.

Wakizungumzia huduma za benki hiyo, baadhi ya wateja walisema imekuwa mstari wa mbele katika kuwasaidia kutatua changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo katika shughuli zao za kila siku. "Nimejenga nyumba zangu kupitia mikopo ya benki hii na kwa hilo nawashukuru sana,'' alisema Maulid Kitenge.

# Mjadala lugha ya kufundishia wahitajika

**Na Vincent Mpepo,** OUT

KUTOKANA na changamoto ya kutokuwapo kwa msimamo wa nchi kisera, kisheria na kiutekelezaji kuhusu lugha ya kufundishia, wadau wa elimu wameona kuna umuhimu kuwapo kwa mjadala utakaotoa hatima kuhusu jambo hilo.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na washiriki wa warsha ya uandishi wa kitaaluma inayofanyika jijini Dar es Salaam, ambapo waliona kutokuwa na sheria, sera na taratibu za kiutkelezaji kuhusu lugha ya kufundishia kunalifanya taifa kukosa dira kimtizamo kutokana na mkanganyiko wa lugha ya kufundishia nchini. Mkurugenzi, Kurugenzi ya Utafiti, Machapisho na Uvumbuzi Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Prof. Emmanuel Kigadye, alisema kuna haja ya kuwa na mjadala wa kitaifa utakaosaidia upatikanaji wa maoni, ili kufanya maamuzi kuhusu jambo hilo.

Akichangia mada hiyo, Prof. Mugyabuso Mulokozi, alisema jambo hilo linatokana na kasumba ya kuamini lugha za kigeni wakati kiuhalisia ujifunzaji kwa lugha ya Kiswahili ndiyo njia sahihi katika kusaidia upatikanaji wa maarifa na ujuzi wa fani mbalimbali kwa watanzania wengi.

"Mafundi katika fani mbalimbali, ambao wamesomea ufundi ikiwamo VETA, wanatengeneza magari, mashine, wajenzi wa maghorofa na miundombinu hawahitaji lugha za kigeni kufanya mambo hayo bali maarifa na ujuzi," alisema Prof. Mulokozi.

Alisema mjadala wa lugha ya kufundishia ni wa muda mrefu, lakini bado kama nchi hatujafikia muafaka wa kuamua nini tukifanye kazi matokeo yake ni kuwa na aina ya watumia lugha ambao siyo mahiri kwenye Kiswahili au hata hizo lugha za kigeni.

Alisema umefika wakati ambapo kama nchi, tunapaswa kutambua thamani ya lugha ya Kiswahili, akisisitiza kuwa kufundisha kwa Kiswahili haimaanishi tuna uwanja finyu kwani tunaweza kufundisha lugha nyingine pia. Mhadhiri wa Sheria OUT, Dk. Abdallah Mlindoko, alisema tatizo lipo kwenye mifumo ya kisheria na kisera ndani ya nchi ambayo haina msisitizo kuonesha utekelezaji wa jambo hilo.

"Mfano wenzetu Rwanda walikukusudia kuachana na Kifaransa wakaweza kwa kupeleka Wanyarwanda wengi kusoma na wamefanikiwa kujijenga kimatumizi ya lugha ya Kiingereza, kwanini sisi tushindwe?" Alihoji Dk. Mlindoko.



Wananchi wa Kitongoji cha Zunga, Kata ya Msata katika mji wa Chalinze, mkoani Pwani, wakifurahia huduma ya majisafi baada ya kujengewa kioski cha majisafi cha umma na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), ambapo wananchi zaidi ya 300 wananufaika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watakaochoma moto misitu sasa kukiona

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, ameagiza kukamatwa kwa watu wenye tabia ya kuchomo moto ovyo katika maeneo mbalimbali yakiwamo ya misitu na mashamba.

Alitoa agizo hilo jana baada ya kukagua shamba darasa la mkulima katika Manispaa ya Tabora, na shamba la uzalishaji wa mbegu za korosho linalomilikiwa na Taasisi ya Utafiti Tanzania Tawi la Tumbi mkoani hapa.

Dk. Sengati alisema uchomaji wa moto unasababisha hasara kubwa kwa mkoa na watu binafsi kwa kuharibu mistu ya asili hata mashamba ya watu yakiwamo ya mikorosho, hivyo kusababisha warudi nyuma kiuchumi.

Aliwataka viongozi kuanzia ngazi za wilaya hadi vitongoji kuhakikisha wanasimamia zoezi hilo la kukabiliana na watu hao kwa kuwakamata na kuwapa adhabu kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Kwa mujibu wa Sengati, moja ya adhabu ambayo wanatakiwa kutoa ni na kuhakikisha wanapanda miti kufidia hasara waliyosababisha ili iwe fundisho kwa watu wengine.

Katika hatua nyingine Mkuu huyo wa Mkoa ameziagiza halmashauri zote kuhakikisha zinakuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji katika mkoa huo.

Alisema ni lazima maeneo ya kilimo na yale ya malisho ya mifugo yajulikane, ili kudhibiti kuingiliana kunakosababisha migogoro.

ama
ALHAMISI OKTOBA 8, 2020
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**Hesabu ngumu: Ubia ongezeko la joto, moto, kujaa hewa chafu**



Ukurasa 12

**Siku ya Makazi Duniani inatubebesha uhalisia wa maboresho ya tunakoishi**



Ukurasa 13

Simulizi kuu za aliyepona Saratani Titi

# Hadhi ya mzee na haki kuu inayompasa mezani kwake

**Na Sabato Kasika**

NI wiki iliyopita tu, kulikuwapo maadhimisho ya Siku la Wazee Duniani. Inawezekana ukachukuliwa kuwa jambo la kawaida, hasa kwa wasio na umri huo na si mashuhuda kamili kuhusu kinachowajiri.

Hata hivyo bado kunadai jibu kwa swali Mzee ni nani? Inawezekana ikawa jambo lisilohitaji ufafanuzi, kwani kila mmoja anaelewa fika, kwamba kila mmoja kama asipoushuhudia kushoto, basi uko kulia ndani ya jamii anayoishi kwa kutumia uzoefu.

Kwa tafsiri ya kifafanuzi, uzee na kuzeeka ni hatua ya mwisho ya makuzi ya binadamu, ambayo mchakato wake unaanzia utoto, ikifuatiwa na ujana. Sifa kuu ya mzee hasa kiafya, huwa anapungukiwa nguvu za kufanya kazi, kulinganisha na alikotoka ujanani.

Hata hivyo, katika sura ya pili jamii ya hao wasio na nguvu mwilini, upeo na busara zao kifikra ziko juu zaidi, katika ngazi kuu.

Mtu anapofikia hatua hiyo ya umri mkubwa, uwezo wa kumudu gharama za maisha unapungua. Hapo inahusu pia kugharamia afya, hivyo kubaki kuwa wa kusaidiwa na watoto familia na jamii kwa ujumla.

Nchini, hadi sasa mamlaka za kiutawala zimeshaliona hilo kwa waliofikisha umri wa miaka 60 na zaidi, wanapaswa kisheria kupata huduma za afya bila ya malipo katika vituo vyote vya afya vya serikali, ili kuwawezesha kuendelee kutetea afya zao.

Hiyo ni kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003, inayoelezea kwa kina sababu za kuwapo kwake kutokana na uzoefu wa mazingira, kusimamia mwongozo wa utoaji huduma za afya.




Baadhi ya wazee walioshikilia bango lenye ujumbe kupinga unyanyasaji dhidi yao, kwenye maandamano ya hafla inayowahusu Kariakoo, mjini Unguja. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Sera ya Taifa ya Wazee inawatambua kuwa rasilimali muhimu katika maendeleo ya taifa, kwa kuwashirikisha katika uamuzi muhimu unaowahusu kwa ujumla wao.

Suala la kushirikisha jamii hiyo katika uzalishaji mali, kufikia hatua ya kuondoa umaskini miongoni mwao na kuboresha huduma zinazotolewa kwa wazee, kutoa ulinzi wa kisheria katika sura ya wao ni kundi maalum.

Vilevile, sera inalenga kuwaelimisha vijana kuhusu masuala ya uzee na kuzeeka na kuwajengea uwezo wa kufanya maandalizi ya maisha kuelekea



Mzee Nassor Salum Hamad, mkazi wa Dunga Kiembeni, Unguja.

uzeeni, kwa kuwa kila mmoja ni mzee mtarajiwa, pindi atakapojaliwa kufikia umri huo.

Ndani ya Sera ya Taifa ya Wazee, serikali inaweka wazi kuwatambua kwamba ni rasilimali na hazina kubwa kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Aidha, inaitaja nchi kuwa kielelezo tosha cha mchango mkubwa wa wazee walioutoa katika nyanja kama za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

Ni miogoni mwa sababu zinazohalalisha kutambuliwa kwao, hata ukazaa kuwapo kwa sera hiyo, ili wazee waendelee kupata huduma za afya bure kwenye vituo vya afya vya serikali.

Ingawa kuna changamoto mbalimbali katika utoaji huduma za afya kwa wazee, ni vyema kukiri uwapo wa juhudi zilizofanyika zikiwamo kuwapa vitambulisho vinavyowawezesha kupata huduma hizo bure.

Ndani ya hayo yaliyo chanya, kuna viashiria vya sehemu ya upungufu kama kukosekana dawa katika vituo vya afya, huku wakielekezwa na baadhi ya wahudumu wa afya kuwa wakanunue katika duka za dawa.

Mtazamo na mkakati ulioko kiserikali, ni kuongeza idadi ya wazee waliopatiwa vitambulisho vya kuwawezesha kupata matibabu bure, kutoka wazee 213,025 katika miaka mitano iliyopita hadi 1,042,403.

Pia, kunatajwa mengine kama vile kuongeza makazi yanayomilikiwa na serikali kufikia 16 na kuimarisha upatikanaji huduma za afya kwa wazee hao.

MAZINGIRA

WAZIRI LUKUVI:

# Siku ya Makazi Duniani inatubebesha uhalisia wa maboresho ya tunakoishi

**Na Mwandishi Wetu**

MWEZI Desemba ya mwaka 1985, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, liliazimia kila Jumatatu ya kwanza ya mwezi Oktoba ya mwaka, itakuwa maalum kwa ajili ya kuadhimisha masuala ya makazi, ikibatizwa "Siku ya Makazi Duniani."

Ni nchi wanachama wa umoja huo chini ya utaratibu wa Shirika la Makazi Duniani (UN-HABITAT), zinaaadhimisha kwa njia mbalimbali, ikiwamo kutafakatri hali ya makazi katika nchi na matatizo yake, kisha inapangwa mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo.

Kila inapofika tarehe 5, mwezi Oktoba, Tanzania inajumuika kimataifa kuadhimisha Siku ya Makazi Duniani, yanayotoa fursa kwa kila taifa na wadau wengine wa makazi kutafakari nafasi zao wanavyoshiriki kuboresha hali ya makazi katika miji yao.

Tanzania inatajwa kubeba wajibu wa maisha kijamii, katika mtazamo kuwa maeneo yake mengi yanazidi kuongezeka ukubwa, idadi ya wakazi na vijiji vinapanuka, hata kugeuka kuwa miji.

Siku ya Makazi Duniani inaongozwa na kaulimbiu ya mwaka husika, kutafakari kwa kina suala husika, jambo linalotoa fursa na mazingira wezeshi ya kutafuta ufumbuzi kwa muda mfupi, pia muda mrefu kwa suala husika mwaka huo; Kaulimbiu ya mwaka ni 'Nyumba kwa wote, Miji bora ya Baadaye.'

Nyumba ni sehemu muhimu ya mahitaji ya msingi ya binadamu, haki inayotambuliwa kitaifa na kimataifa.

Pia, kuna matamko na mikataba inayotambua haki hizo za msingi, ikijumuisha Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu la mwaka 1948 na 1966 na Tanzania imeliridhia.

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000, pia inatoa mwongozo unaoipa kipaumbele sekta ya nyumba, katika kuwezesha upatikanaji nyumba bora na za gharama nafuu kwa wananchi wa vipato mbalimbali.

Nyumba inatajwa kuwa kigezo kikuu cha kukuza uchumi na udumishaji amani katika nchi yoyote. Uwekezaji katika sekta hiyo unachangia moja kwa moja ukuaji wa mitaji, ajira, kipato, akiba, kuimarisha afya na elimu.

Serikali zote duniani, kwa sasa zinathamini mchango wa sekta ya nyumba katika ukuzaji uchumi na kichocheo katika kudumisha wa amani, hivyo inatoa udhahiri kwamba hakuna nchi inayoendelea, pasipo kutoa kipaumbele katika sekta ya nyumba.

Ukuaji wa sekta hiyo unatajwa kuchangiwa na uwekezaji unaofanywa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi.

**MAGEUZI NCHINI**

Pamoja na sekta hiyo kukua taratibu, kunaelezwa kuna jitihada zinazofanywa na serikali kuhakikisha kuwa sekta hiyo inakuzwa nchini, mathalan miaka mingi ya kuwapo Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Benki ya Nyumba (iliyofungwa), Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa watumishi wa serikali na kuanzishwa Kampuni ya Watumishi Housing (WHC).

Aidha, juhudi nyinginezo ni ktungwa sheria kadhaa kama vile ya Mikopo ya Nyumba; Sheria ya Miliki ya ya Jengo ya Mwaka 2008, sambamba na miradi na mifuko inayowezesha maendeleo ya sekta ya nyumba kama vile Mradi wa Mikopo ya Nyumba na Mfuko wa Mikopo Midogo ya Nyumba.

Kupitia Mradi wa Mikopo ya Nyumba, ulio chini ya mradi wa benki na taasisi za fedha, zimekuwa zikipatiwa mitaji jili ya kutoa mikopo ya nyumba kupitia asasi ya Tanzania Mortagage Refinance Company (TMRC).

Hivyo, inaimarisha upatikanaji mikopo ya ujenzi au ununuzi wa nyumba na katika kukabiliana na changamoto zilizopo, kwenye sekta ya nyumba na kuwezesha mazingira ya upatikanaji wake kwa gharama nafuu.

**SEKTA INAKOELEKEA**

Kimsingi, kuna hatua mbalimbali za kuandaa sera mpya ya nyumba, inayotoa dira ya uendelezaji sekta hiyo nchini, ikiwamo kubuni mbinu mbalimbali zinazowawezesha wananchi wa kipato cha chini kupata nyumba bora.

Aidha, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais (TAMISEMI), inaahidi kuendelea kutekeleza miradi ya urasimishaji nchini, kwa kutambua miliki kwa hatua, ili kuyaweka maeneo yenye makazi holela, yanapata huduma za kiuchumi na kijamii, kupitia mpango shirikishi.

"Miradi hii itaendelea katika miji mbalimbali nchini kwa lengo la kuboresha hali ya maisha ya makazi husika na kupunguza umaskini," anaeleza Waziri mwenye dhamana na Ardhi, William Lukuvi na anaendelea:"Faida nyingine ni pamoja na kuongeza usalama wa miliki kwa kutoa hati miliki za ardhi,"

Katika salamu zake za Siku ya Makazi Duniani, Lukuvi anasema, Wizara ya Ardhi iko katika maandalizi ya kufanya sensa ya nyumba, kutambua idadi kamili ya nyumba na kusaidia kubaini uhaba na hali ya nyumba.

Anasisitiza kuwa, matokeo ya sensa hiyo yatasaidia kuandaa mipango mikakati ya maendeleo ya nyumba na katika kinachooneka kuzingatia umuhimu wa nyumba kwa kila mwananchi.

Waziri Lukuvi, aliziagiza ofisi za ardhi za mikoa yote na mamlaka za upangaji, kusimamia kikamilifu utambuzi , upangaji, upimaji na miliki ya makazi kwa kufuata sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyotolewa, ili kila mwananchi mwenye kiwanja na nyumba katika sehemu zinazokubalika kisheria, aweze kumilikishwa.

Aidha, anazitaka halmashauri zote kuwapatia waendelezaji miliki huduma watakazohitaji, kama vile kuanisha maeneo yanayofaa, ipewe mipango ya uendelezaji miji, upimaji viwanja, kuweka miundombinu.

Kwa mujibu wa waziri, halmashauri pia zinapaswa kutoa hatimiliki za ardhi na vibali vya ujenzi kwa wakati na kukagua utekelezaji miradi ya ujenzi.

Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi,katika hitimisho la salamu zake za Siku ya Makazi Duniani, anawataka wananchi kuitumia siku hiyo kutafakari mada mbalimbali na kuzijadili kwa kina, kuona namna chachu ya mabadiliko chanya katika masuala ya sekta ya maendeleo ya nyumba nchini.



Mkurugenzi wa Idara ya Umiliki wa Mamlaka ya Majengo, Bartazari Kimangano (wa tatu kushoto), akiongoza msafara wa wakuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kukagua baadhi ya nyumba za umma, Bunju, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wiliam Lukuvi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

AFYA

MAPINDUZI HOSPITALINI OCEAN ROAD

# Simulizi kuu za aliyepona Saratani Titi

- Mapya; tiba bila upasuaji, kwa mwaka 100
- Mkurugenzi: Wataalamu wananolewa China
- Mafanikio juu, kikwazo ni mitandao ya jamii

**Na Mary Geofrey**

"KUISHI miaka 18 nikiwa mwenye saratani ya titi siyo jambo rahisi hata kidogo. Ni Mungu aliyenisaidia na nafsi yangu kukubaliana na majibu ya daktari," anaanza kusimulia Halima Mwaipopo, aliyetibiwa na kupona Saratani.

Anasimulia uzoefu wake, kukutana na unyanyapaa kupindukia kutoka kwa wanaomzunguka, familia, ndugu, jamaa na marafiki, akisimulia:

"Walikuwa wakija kuniona, wanasema 'mhhh huyu basi tena, hawezi kupona, hakuna aliyeugua Saratani akapona huku ni kifo tu! Na wakati mwingine walikuwa wakiyazungumza mbele yangu'" anasimulia Halima.

Anaeleza kilichompa ujasiri aliekelekea imani yake zaidi kwa Mungu, huku akiwawasilikiza na kufuata ushauri wao madaktari waliomtibu.

"Ugumu ukaja wakati natakiwa kukatwa ziwa, kila mtu alinishauri usiende kwanza, subiri huo ni uamuzi mgumu, huwezi kupona tena. Niliziba masikio, nikabaki kusikiliza tu nini anachonieleza daktari wangu," anasimulia Halima mama wa watoto watatu.

Anaeleza wakati anapitia changamoto ya ugonjwa alikuwa na mtoto wa miaka minne aliyemtegemea kwa mengi na akalazimika kukaa naye mbali, ili ashughulikie kwanza afya yake.

"Niliondoka na kuacha familia yangu pamoja na mwanangu mdogo kuja Dar es Salaam, kufuata matibabu, wakati ambao sikuwa na mtu wa kunifariji zaidi ya kujifariji mwenyewe kuwa nitapona.

"Jambo lililonishtua moyo wangu na kuniondolea ujasiri kwa muda, ni baada ya chumba nilichokuwa nimelazwa kufanyiwa upasuaji kukuta wenzangu wawili wamefariki dunia. Niliumia sana, lakini sikuwa na namna zaidi ya kuendelea kujipa moyo hata kama nikifa ni kwa mapenzi ya Mungu," anasimulia.

Anafafanua kwa sasa mtoto wake ni mtu mzima anayefanya kazi, ilhali naye anaendelea kuhudhuria kliniki katika Taasisi ya Saratani Ocean Road, licha ya kupona, ili isimrudie tena.

### MAGEUZI OCEAN ROAD

"Tunashukuru Mungu Ocean Road ya sasa si kama ile ya zamani. Tulikuwa tunapiga 'kwata'(kusubiri) hapa, asubuhi hadi jioni bado mtu hujapata matibabu, Lakini nilivumilia.

"Leo hii vipImo vya uchunguzi ni vya kisasa, dawa za kutosha kwa kweli inatia sana faraja kwa sisi wagonjwa," anafafanua Halima, akidokeza mageuzi yaliyoko katika miaka mitano iliyopita.

Sasa anajigamba: "Mimi ni shujaa, mimi ni Malkia wa nguvu, ninaweza kuwa sehemu ya kuelimisha jamii, nimeweza kupona saratani na sasa ni mzima nina nguvu, nina furaha na amani tele."



Mashujaa (wanawake waliotibiwa na kupona saratani ya matiti) na wanaoendelea na matibabu dhidi ya saratani, wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI) Dk. Julius Mwaiselage na Mkurugenzi wa Huduma za Kinga wa ORCI, Dk. Crispin Kahesa (mweye tai nyekundu ) wakishiriki kuinua mkono, ishara ya kuishinda.

### KUGUNDULIWA TATIZO

Halima, mkazi wa Masasi, mkoani Mtwara, alibaini kuwa na saratani ya matiti mwaka 2002, baada ya kujichunguza baada ya kubaini tatizo hilo kutokana na uchunguzi aliyofanya kwa njia ya kupapasa maziwa yake.

Hiyo ni baada ya kusikia maelekezo ya kitaalamu redioni, huku akifafanua mwanzo wake: "Nikiwa nyumbani, nilifungulia redio nikakuta kipindi kipo katikati, lakini daktari alieleza namna ya kupima na kujigundua mwenyewe kama una saratani ya matiti, kupapasa maziwa yako ukiwa umelala chali."

Anasema, aliendelea kusikiliza kwa makini maelezo ya daktari aliyetaja kwa jina la Dk. Ngoma (aliyekuwapo Ocean Road) na alianza kujichunguza kama alivyoelekezwa, ndipo aligundua titi lake la kulia ana uvimbe.

"Katika ziwa la kushoto hakukuwa na kitu nilichotilia shaka, lakini nilipohamia ziwa la kulia, nilipopapasa nilihisi lilikuwa na kiuvimbe.

"Sikuwa nahisi maumivu yoyote, nilipokwenda kulala usiku, nilijikagua tena, ziwa la kushoto lilikuwa sawa ila la kulia nilikuta kile 'kiuvimbe' bado kipo," anasimulia namna alivyoanza kujiuliza uhalali wa uvimbe huo kiafya, safari ikirejea somo la Dk. Ngoma na siku iliyofuata alienda hospitali kwa ajili ya uchunguzi.

"Nilikwenda Hospitali ya wilaya, walinikagua na kusema ni uvimbe wa kawaida, sikukubaliana nao. Nilipotoka hapo nilienda tena Hospitali ya Ndanda, nilikutana na daktari (kwa sasa ni marehemu), aliniuliza swali, kwanini nafikiri 'kauvimbe kale' ni saratani. Nilimueleza kwa sababu nilimsikiliza daktari kwenye radio.

"Kwa hiyo, nataka nihakikishe afya yangu, kama ni wa kawaida au saratani, ikigundulika ni saratani basi utolewe mapema," anasimulia kwa kina," Halima anaeleza.

Mama hiyo anafafanua, daktari alichukua sampuli ya kinyama, iliyosafirishwa kwenda Hospitali ya Rufani ya Kanda KCMC, na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na katika hospitali moja nchini Ujerumani.

Halima anasema, wakati anasubiri majibu ya vipimo baada ya kuchukuliwa sampuli, titi lake lilianza kuvimba katika namna inayofanana na maelezo ya daktari radioni, kuhusu dalili ya saratani.

"Majibu ya sampuli iliyopelekwa Muhimbili na Ujerumani yaliwahi kurudi, nilipigiwa simu niende kuyachukua. Nilijipa moyo maana nilikuwa na watoto wadogo, nawalea mwenyewe, kwa sababu nilishatengana na mume wangu kabla hata ya kuanza kugundua tatizo.

"Kwa hiyo, sikutaka kukata tamaa, kila nilipowaangalia wanangu kama mama nilihisi roho inaniuma. Nilienda hospitali nikiwa nimembeba mwanangu wa mwisho, wakati ule alikuwa na miaka minne," anasimulia mkasa ulivyo.

Anasema alipokutana na daktari, alisita kumpatia majibu ya vipimo vyake, wakati ule alikuwa wanataka ndugu wa karibu wa mgonjwa, apatiwe majibu kwa niaba yake.

"Nilivaa ujasiri, niliwaambia pale hospitalini, mimi ndiye mgonjwa wanieleze, maana hata kama atakwenda ndugu yangu, hataweza kunisaidia kwa lolote isipokuwa mimi.

"Walinielewa wakanipa majibu yangu kwamba nina saratani, natakiwa kwenda Ocean Road, Dar es Salaam kwa matibabu zaidi. Kwa kweli, binadamu kupokea tatizo ni changamoto, lakini binafsi nilipokea," anaendeleza simulizi.

### KILICHOJIRI OCEAN ROAD

Anasimulia kwamba, alisafiri hadi jijini Dar es Salaam, alikofika Ocean Road na kukutana na Dk. Ngoma mwenyewe, aliyemueleza anatakiwa kufanyiwa matibabu aina mbili, mionzi inayofanyika hospitalini hapo na kukatwa ziwa, huduma inayopatikana katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).



Halima Mwaipopo, shujaa aliyeishinda kansa.

Halima anasema, alilazimika kuieleza ofisi yake aliyokuwa akifanyia kazi, ambayo walimsaidia fedha za matibabu, safari na chakula wakati wote akiwa kwenye matibabu, hali iliyomtia moyo wa kujaliwa.

### MAGUMU ALIYOYAKUTA

Mama huyo ana simulisi ya ugumu wa kwanza kisakolojia ni pale Muhimbili, ni katika wodi aliyolazwa, kinamama wenzake wawili waliofanyiwa upasuaji saratani ya titi, walifariki dunia.

"Ndugu zangu nilioambatana nao siku ile, nao walishtuka, wakaniuliza itakuwaje?... Siku ya upasuaji ilipowadia, waligoma kuondoka, walikuwa wanalia," anaeleza.

Halima, anaeleza ni kwamba daktari mhusika alilazimika kutumia mbinu ya kuwaondoa, akiwaeleza upasuaji utafanyika saa tisa jioni na walipokubali kuondoka, alichukuliwa na kupelekwa chumba cha upasuaji kuhudumiwa, akikumbuka ilikuwa mwezi Desemba, mwaka 2002.

Anasema, alihudumiwa huku hospitalini hapo kulikuwapo mgomo wa madaktari na anaeleza kumshukuru Mungu, ukiwa upasuaji wenye mafanikio.

Halima anasema, ndugu zake waliporudi mchana, walidhani bado hajaingizwa chumba cha upasuaji, kumbe la hasha, tayari alishafanyiwa upasuaji na kurudishwa wodini.

"Fahamu zilikuwa zimeshanirudia, nilikuwa nawaita majina, walipoambiwa nimeshafanyiwa upasuaji kuondoa titi kwa mafanikio, ghafla walianza tena kulia.

"Walilia mno, niliwauliza kuna msiba? Basi, manesi ilibidi wawatoe, wasinisumbue. Niliwasihi wasilie tena, nimeshafanyiwa upasuaji, niko salama kabisa," anasimulia. Huku akitoa tabasamu.

### USHAWISHI KUTOROKA

Halima anasema, hatimaye aliruhusiwa kutoka hospitali Muhimbili na akarudishwa Ocean Road kwenda kuanza tiba ya mionzi (radiotherapy) na ile ya kemia (chemotherapy), mwaka 2003. Hapo ndipo alipokutana na ushawishi akatoroka tiba.

Anasema wakati anatabitiwa, ndugu na jamaa zake walimtamkia hatoweza kupona, kwa sababu ya madai hasi yaliyopo kuhusu saratani, akiwa na simulizi: "Wengine walinishawishi niachane na matibabu ya hospitali, niende kwa waganga wa kienyeji kwamba nimerogwa, lakini sikukubaliana nao.

"Niliendelea kufuatilia maelekezo ya daktari, nile nini, nifanye nini, mwenyewe niliamua kupunguza

Endelea Uk. 14

MAZINGIRA

# Hesabu ngumu: Ubia ongezeko la joto, moto, kujaa hewa chafu

## •Barafu mlimani inayeyuka, bahari inajaa

**Na Michael Eneza**

MOTO usio na kiwango cha mfano inaendelea katika maeneo mbalimbali duniani, hasa katika jimbo la California nchini Marekani; ukanda wa Siberia nchini Russia; misitu ya Brazil; ukanda mpana Mashariki ya Australia na kwingineko.

Inatajwa tayari imeshaleta utata mpya kuhusu kasi ya madhara ya uzalishaji hewa chafu ya ukaa au kitaalamu 'carbon dioxide.'

Wakati mkakati wa jadi kuhusu suala hilo ni hewa ya ukaa inayozalishwa viwandani au katika matumizi ya vyombo vya usafiri, sasa kuna ya ziada. Hapo kunatajwa kuungua misitu na kuyeyuka barafu, kunatajwa kunaleta hatari ya madhara ya haraka?

Mtu akiangalia kinachosemwa na wataalamu katika taarifa za taasisi tofauti za utafiti zinazotumiwa na wachambuzi wa habari hasa za mazingira kwa mashirika tofauti ya habari, bado hakuna mtiririko mmoja wa tafsiri ya hali hiyo.

Kinachoonekana kwa mfuatiliaji asiyeshiriki katika hisia za kitaaluma zinazotangulizwa, wataalamu wanafanya kila juhudi kuendeleza mikakati ya kisayansi na kisera waliyozoea au inayotawala mwelekeo uitwao 'convention' (makubaliano) katika, tofauti ya mataifa yaliyopo. Mojawapo ni kuwapo 'nishati endelevu' hadi ifikapo mwaka 2030.

### HEWA CHAFU

Baadhi ya tafiti zinaonyesha kujikanganya au kujipinga zenyewe, kwani jitihada ya kipelelezi au kitafiti inayotajwa mwanzo na nyenzo zinazotumiwa, kwa mfano kuandaa vielelezo wima vya mwenendo wa mabadiliko ya uzalishaji hewa chafu kuanzia mwaka 1000 hadi sasa.

Ziko aina tatu za hewa zinazofuatiliwa zaidi, yaani hewa za 'carbon dioxide', methane na nitrous oxide, licha ya kuwa na umuhimu mkubwa wa kuifunika dunia kwa mvuke wa joto unaozuia mionzi hatarishi ya jua, isiifikie dunia.

Hapo zinaweka ukanda wa kufyonza nguvu za mionzi ya aina tofauti na kupitisha kidogo huku kilichobaki na sehemu ya joto la dunia, hurushwa na kurudi katika anga za juu.

Jarida moja la nchini Marekani, linamnukuu mwanasayansi Peter Tans, anayeeleza kujali kinachotokea hivi sasa, ingawa anaamini tofauti kati ya dunia iliyofunikwa na barafu na hali ya sasa nyuzi joto kidogo ya ziada.

Hapo ndipo kunazuka mdahalo usioisha wa wanasayansi duniani na hasa nchini Marekani, baadhi wakidai hakuna ongezeko la jumla la joto duniani, kwani anga za juu zinapopokea joto la ardhini na kupitia mchakato wa kujipunguza yenyewe.

Pia, kuna wanasayansi wanaolikataa hilo, wakisema kuna ongezeko a kiwango cha joto kwa kasi kubwa.

### MATUKIO MOTO

Wapo wanaounganisha na kuwepo matukio ya moto, ni zao la joto linalojenga mazingira chanya ya kuibuka moto, hali inayojidhirisha zaidi katika nchi kama Marekani na Brazil, vivyo hivyo kuna wengi wanaobakiwa na maswali yasiyo na majibu katika hilo .

Yapo maeneo ya kisayansi yanayozidisha ubishi huo, mfano kwa kiwango gani cha moto nchini Marekani, umesababishwa na kuongezeka joto, au ni watu kuanzisha moto ya hapa na pale.

Rais Donald Trump, katika falsafa yake kisayansi inayoungana na siasa za chama chake, Republican, alikataa dhana hiyo katika mdahalo na mshindani wake Joe Biden, wa chama cha Democratic.

Kwa mujibu wa Rais Trump, shida ya kuibuka moto kia mara ni udhibiti mdogo kutoka jimboni California, kunakoshikiliwa na wapinzani wa Democratic.

Ushindani wa jumla wa Rais Trump katika utawala wake dhidi ya wataalamu mazingira, ambao kwa asilimia wanaegemea chama cha Democratic, ni haja ya kuwapo mizania sahihi ya uwezo wa kunyonya joto na kasi ya kulitupa angani.

### WANAMAZINGIRA

Wanamazingira wanapigania hoja ya kuhakikisha kunapunguzwa 'shughuli za binadamu' zinazosababisha uharibifu mazingira na hasa viwanda kutumia makaa ya mawe, mafuta ya petroli, dizeli au mafuta mazito (machafu) na miaka ya karibuni, kuna kampeni dhidi ya matumizi ya plastiki.

Hadi sasa kuna tetesi za kuwapo kampuni inayounda teknolojia ya kuzungusha upya plastiki, ziwe inaharibika ardhini isidumu muda wote, hivyo kuondoa uharibifu wake mkubwa wa mazingira.

Rais Trump na wafuasi wake kama Rais Jair Bolsonaro wa Brazil, wanatanguliza kwanza ulazima wa viwanda, wakipuuza dhana ya kuongezeka nyuzi joto na kuwapo moto.

Watafiti maeneo ya barafu katika duniani, wana ushuhuda wao kuhusu namna mabonge ya barafu yanavyoyeyuka kwa haraka na hakuna utafiti wa kuunganisha mzizi wa viashiria hivyo.

Mtazamo wa sasa unaonyesha namna milima ya barafu itayeyuka kabisa hadi kufika mwisho wa karne iliyoko'ilhali hakuna uchambuzi wa kina kimazingira unaohusiana na kuongezeka nyuzi joto duniani, ukijidhihirisha kupitia matukio kama vimbunga na mafuriko.

Mtazamo huo, ndio unatawala katika siasa za ughaibuni na hususan nchini Marekani, hata ushuhuda wa kinachoendelea katika mijadala ya televisheni, wagombea urais wa Marekani wanavyosutana na kuitana majina ya kashfa.

Ni mkanganyiko wa imani katika jamii ya Marekani, kwani mzozo huo unaonekana pia katika kutafsiri janga la Covid-19, mathalan kundi la Rais Trump, linaona ni la kupita na wanaona la msingi ni uchumi ufunguliwe, kila mtu achukue tahadhari anazopenda.

Waliobaki wanasema si suala la kila mtu kuchagua, kwani kutomjali mtu mmoja mmoja ni janga kwa wengine.



Tukio la moto nchini Marekani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# Simulizi kuu za aliyepona Saratani Titi

**Inatoka Uk. 13**

kula nyama nyekundu maana nilishasikia nyama nyekundu zenye mafuta mafuta, niliamua kula samaki, kunde, mboga za majani, huku nikiendelea kumuomba Mungu anisaidie watoto wangu wakue, maana najua kifo tumeumbiwa binadamu."

### MATIBABU NCHINI

Mkurugenzi wa Huduma za Kinga wa ORCI, Dk. Crispin Kahesa, anasema takwimu za taasisi ya Globalcan mwaka 2018, inakadiria wastani wagonjwa 42,060 wa saratani wanagundulika kila mwaka nchini, Tanzania, kati yao asilimia 7.2 ni matiti.

Anasema nchini takwimu zinaonyesha kuwa, mwaka 2018 wagonjwa wa saratani waliohudhuria hospitali ni zaidi ya 12,215 kati ya 42,060 wanaokadiriwa kuwapo. Pia, takwimu zinabainisha kinamama wanaougua saratani ya matiti, jumla yao ni asilimia 16 ya wagonjwa wote, huku Dk. Kahesa akisistiza takwimu zaonyesha saratani hiyo ya matiti ni tatizo kubwa inayoshika nafasi ya tatu kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa kitaifa, ikitanguliwa na kizazi, pia tezidume.

Daktari huyo bingwa anasema, wastani wa umri wa wanawake wanaogundulika kuugua unashuka, akiwa na takwimu za mwaka 2008/09, wanawake waliokutwa wanaugua walianzia miaka 64 lakini miaka 10 baadaye, 2019 walianzia miaka 56 na wapo hadi wenye umri miaka 25.

Anasema takwimu hizo ni kiashiria cha hatari, kwamba saratani sasa imeanza kushambulia hadi wanawake wenye umri mdogo.

### MAGEUZI MAKUBWA

Mkurugenzi Mtendaji wa Ocean Road, Dk. Julius Mwaiselage, anasema miaka 10, ilishika nafasi ya nne kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa nchini, ili hivi imejiwekea kuwa ya pili.

Anataja sababu mojwapo ni wimbi la taarifa potofu, hasa katika mitandao ya kijamii, baadhi ya wagonjwa wanashawishiwa kukimbilia dawa za kienyeji, ambazo hazijatifatiwa kitaalamu, ikikadiriwa wanafikia asilimia 10 ya wagonjwa wa saratani zote.

Dk. Julius Mwaiselage, anasema wagonjwa hao wengi huondoka katika mtindo wa kutoroka wodini, akifafanua kuna wanaopoteza maisha huko na wachache wanaorudi, huwa wameathirika kwa kiwango cha juu.

### MAGEUZI MAKUBWA

"Tunasisitiza wazingatie matibabu, hata wakienda huko, wasiache matibabu. Serikali inazidi kuboresha huduma, sasa tunao uwezo wa kuigundua mapema na kuitibu pasipo kuondoa titi lote, ikiwa mtu atagundulika mapema.

Anasema kila mwaka wanatibu kwa upasuaji pasipo kuondoa titi wastani wa wanawake 100, sawa na asilimia 30 ya wagonjwa wote wanaowatibu kwa mwaka.

"Hata wale waliofanyiwa upasuaji na kuondolewa katika titi lote jitihada zinafanyika. Wataalamu wetu wapo China wakijifunza jinsi ya kufanya upasuaji wa kupandikiza matiti, walikuwa wawe wameshamaliza masomo yao na kurejea nchini tayari kuanzisha huduma hii, corona imetucheleweshа," anasisitiza.

Katika miaka ya karibuni, kumekuwapo mageuzi makubwa katika Taasisi ya Saratani Ocean Road, kwa kuwekewa vifaa vya kisasa, maabara na majengo mengine kuongezwa, pia wataalamu, hali iliyofuta foleni na adha ambazo mgonjwa Halima anazitaja kukutana nazo, alipokuja mara ya kwanza wastani wa miaka 18 iliyopita.



# Mamilioni ya vitabu elimu yasambazwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

VITABU vya kiada 1,175,300 vya shule za sekondari na 21,179,652 vya shule ya msingi, vimechapishwa na kusambazwa kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza juzi kwenye Kongamano la Walimu lililofanyika jijini hapa, Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA), Dk. Charles Msonde, alisema hatua hiyo imepunguza uhaba wa vitabu hivyo.

Dk. Msonde alisema serikali ilitoa Sh. bilioni 67.5 ili kuchapishwa na kusambazwa kwa vitabu hivyo.

"Upatikanaji wa vitabu umeboresha elimu katika ngazi zote za elimu na wanafunzi kumudu masomo yao," alisema.

Kwa upande wa wanafunzi wenye uhitaji maalum, alisema vimesambazwa vitabu vya kiada 31,602 kwa shule za msingi na sekondari vitabu 5,100 na kufikia uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja.

Dk. Msonde alisema serikali imejitahidi kuboresha sekta ya elimu kwa kujali shule mbalimbali ikiwamo kugawa vifaa vyote kwa shule hizo. Pia alisema serikali itaendelea kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa shule za msingi na sekondari. Kwa mujibu wa Dk. Msonde, takwimu zinaonyesha kwamba walimu wamekuwa wakifanya kazi kubwa katika maeneo mbalimbali hadi muda wa ziada wa kazi. Naye Katibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Deus Seif, alisema walimu watahakikisha wanafanya kazi kwa bidii ili kuinua sekta ya elimu.

Alisema walimu wana lengo moja la kuhakikisha sekta ya elimu inasonga mbele na si kurudi nyuma ndio sababu walimu wengi wanafanya kazi hadi muda wa ziada.

"Tunajitahidi kuiboresha sekta ya walimu ndiyo maana unaona kila kukicha tunapambana kuhakikisha kazi zinafanyika kwa bidii," alisema.

Kadhalika, aliishukuru serikali kwa kutoa ajira 13,000 za walimu ambazo zitaongeza nguvu kazi na kupunguza mzigo wa vipindi kwa walimu shuleni.

"Pamoja na hizi ajira kuongezwa, serikali isisite kuongeza walimu wengine ili kusiwe na uhaba wowote katika shule za mijini na vijijini," alisema.

Alisema walimu wamekuwa na mikakati mbalimbali ya kuboresha suala ufundishaji ili wanafunzi waelewe masomo wanayofundisha.



Waendesha baiskeli walioshiriki matembezi ya kumuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere kutoka Dar es Salaam hadi Butiama wakifanya usafi kwenye mitaa mbalimbali ya Jiji la Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ofisa masoko abaini shida kwa machinga wa Dodoma

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, amewataka wafanyabiashara wadogo kuhakikisha wanafanya usafi kwenye maeneo wanayofanyia biashara badala ya kusubiri kufanyiwa na jiji.

Yuna aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara hao wakati akikagua maeneo wanayofanyia biashara.

Alisema baadhi ya wamachinga wana tatizo la kutofanya usafi kwenye maeneo yao hata kama kuna faida ambayo wanaipata.

"Nimejionea mwenyewe baadhi ya maeneo ambayo wamachinga wamekuwa wakifanya biashara zao, si rafiki kwa kufanya shughuli zao kutokana na hali ya mazingira kuwa hairidhishi kwa kufanya biashara. Hata kusafisha tu wenyewe ni mtihani kwao," alisema Yuna.

Pia aliwataka kutoa ushirikiano kwa taasisi na watu binafsi wanaojishughulisha na suala la kuweka jiji katika hali ya usafi.

"Pamoja na taasisi hizo na watu binafsi, ni wajibu wao kufanya usafi huo pia wafanyabiashara wana wajibu wa kuhakikisha kwenye maeneo wanayofanyia biashara yanakuwa safi kwa muda wote badala ya kusubiri kufanyiwa," alisema.

Pia aliwahimiza kuzingatia maelekezo ya jiji kwa kuepuka kufanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi ili kutoathiriwa biashara zao.

Alisema maelekezo hayo ni pamoja na kutopanga biashara zao kwenye maeneo ya barabara ambazo muda wote zimekuwa zikitumika kwa kupita vyombo vya moto.

"Jiji halitakuwa tayari kuwaona baadhi yenu mkikiuka maelekezo mliyopewa ya kufanya biashara zenu kwenye maeneo ambayo ni hatarishi kwa upande wa bidhaa zenu, wateja wenu na hata nyinyi wenyewe, hivyo ni muhimu mkaheshimu sheria, kanuni kama inavyoelekeza," alisema.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara hao kushirikiana na jiji wanaogundua kuna baadhi yao wamekuwa wakikiuka maelekezo kutoka ngazi husika,kama vile wale wanaovamia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za kiserikali na kuweka vibanda.

Katika hatua nyingine, Yuna alisema kumekuwapo na baadhi ya wafanyabiashara wanaowalaghai wenzao kwa kuwauzia maeneo ambayo yako wazi huku wakidai kuwa wana vibali halali toka jiji jambo ambalo si kweli.

# Malimao yaadimika, bei yake haishikiki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAFANYABIASHARA katika masoko mbalimbali jijini Dodoma wameeleza kuadimika kwa malimao, hali ambayo imesababisha bidhaa hiyo kupanda bei kutoka Sh. 100 hadi Sh. 500 kwa limao moja.

Aidha, kwa sasa wafanyabiashara wananunua mfuko wa kilo 100 kwa zaidi ya Sh. 250,000 huku upatikanaji wake ukiwa si wa uhakika.

Mfanyabiashara katika soko kuu la Majengo jijini hapa, Haruni Iddy, alisema jana kuwa kwa sasa bidhaa hiyo imekuwa adimu kupatikana na kuwalazimu kufuata nchi za nje kama vile Sudan, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Pia alisema kutokana na mvua kunyesha kwa wingi nchini mwaka huu, msimu wa pili wa malimao haukuwapo hali ambayo imesababisha kutokuwapo kabisa nchini kwa bidhaa hiyo.

Vile vile, alisema kuwa hivi sasa wamekuwa wakiuziwa mfuko wa kilo 100 gunia moja kwa zaidi ya Sh. 250,000 na upatikanaji wake ni shida sana.

"Hivi sasa kupata limao ni shida sana kama hapa unavyo ona limao moja tunauza Sh. 500 wakati kipindi cha nyumba hata ukiwa na Sh.100 unaweza kupata fungu," alisema.

"Zamani mtu ukimwambia unafanya biashara ya malimao anashangaa, lakini hivi sasa hata ukipita barabarani umebaba mzigo wa malimao watu wanakuulizia bei tofauti na zamani. Corona imepandisha sana hadhi ya limao," aliongeza.

Alibainisha kuwa kuwa wakati wa mlipuko wa virusi vya corona nchini bidhaa kama vile malimao, tangawizi pamoja na vitunguu swaumu mahitaji yake yaliongezeka sokoni.

"Wakati wa corona tunashukuru Mungu pamoja na mahitaji kuwa juu, ulikuwa msimu wa malimao pamoja na tangawizi. Kama ingekuwa kama hivi sasa hali ingekuwa mbaya sana kwani malimao ni adimu sana," alisema.

Hassan Chitembedya, mfanyabiasahra wa soko la matunda na mboga la Bonanza jijini hapa, alisema hivi sasa malimao sokoni hayakai kutokana na mahitaji kuwa juu.

Chitembedya alisema pia malimao mengi yanasafirishwa kwenda nje ya nchi kama vile Kenya kama sehemu ya tiba mbadala.

"Yaani sasa hivi sokoni limao halikai kabisa, mimi nilikuwa na mzigo lakini nimemaliza, mahitaji yako juu sana hivi sasa kuliko hata kipindi cha mlipuko wa corona," alisema.





## 90% wajengewa uwezo kutambua fursa Jiji la Mbeya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ASILIMIA 90 ya vijana katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wamejengewa uwezo wa kutambua fursa mbalimbali za kiuchumi na kuzifanyia kazi ili kujikwamua na umaskini, kwa kuamua kujihusisha kwenye shughuli za kilimo biashara na ujasirimali.

Ofisa ufuatiliaji kutoka Shirika la Starve for Helping Other People (Shop) linalofadhiliwa na Shirika la Foundation for Civil Society, Yusuph Simbaya, aliyasema hayo jana wakati wa kikao cha kufanya tathmini juu namna walivyolisaidia kundi la vijana kushiriki kikamilifu kuanzisha shughuli zinakazowasaidia kuendesha maisha yao ya kila siku.

Alisema elimu ya kujitegemea, ujasiriamali, kujitambua na uzalendo imesaidia makundi mbalimbali ya vijana mkoani Mbeya sasa kujikita kwenye kutafuta ridhiki na sio kukaa tena vijiweni.

Alisema vijana sasa wameshajitambua wameanzisha biashara mbalimbali za kuwaingizia kipato ukilinganisha na ilivyokuwa awali ambapo walikuwa tegemezi na kujihusisha na vitendo vya uhalifu ikiwamo wizi, uvutaji bangi na uporaji huku wengine waliomaliza vyuo wakisubiri ajira kutoka serikalini.

"Kiwango hicho cha asilimia 90 kinatokana na utafiti tuliofanya kwa kuwatembelea vijana ambao tuliwapa mafunzo ya kujikwamua kiuchumi kwa kuwafikia zaidi ya 500, licha ya kuwapa elimu lakini tuliwaunganisha na wadau mbalimbali kutoka taasisi za kifedha na masoko," alisema Simbaya.

Aliongeza kuwa waliwasisitiza vijana kuongeza nidhamu ya matumizi ya fedha wanazozipata kwa kuhakikisha wanapanga bajeti zinazoainisha vipaumbele vyao ili waweze kutimiza malengo na kujiletea maendeleo.

Miongoni mwa vijana walionufaika na miradi ya shirika hilo, Shukrani Jackson, alisema awali alikuwa hazitambui fursa za kiuchumi katika eneo lake, lakini kupitia mafunzo aliyoyapata alianzisha biashara ya duka na uuzaji wa mazao ambayo imesaidia kumudu gharama za maisha.

Alisema awali alipokuwa chuoni alidhani akimaliza atapata ajira, lakini ilikuwa tofauti hali ambayo ilimvunja moyo na kukata tama ya maisha lakini baada ya kupata elimu ya kujitambua na ujasiriamali alimua kuanzisha shughuli ambayo hadi sasa inaendesha maisha yake.

Nuru Adam, alisema awali kabla ya kupata elimu hiyo alikuwa akikaa nyumbani bila kujishughulisha na kitu chochote kwa kudhani kuwa wazazi ndio wanajukumu la kumhudumia kwa kumpatia mahitaji yake yote.

Alisema wakati mwingine alitegemea msaada kutoka kwa mpenzi wake ambaye hakuweza kutimiza mahitaji yake yote, hali ambayo ilisababisha kuwa katika mahusiano na wanaume wengi ili kukidhi mahitaji yake.

# Mgombea aahidi kutengea mifugo maeneo ya malisho

**Na Grance Mwakalinga,** MBARALI

MGOMBEA ubunge Jimbo la Mbarali mkoani Mbeya kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi CCM, Francis Mtega, amewaahidi wananchi kuwa endapo atapewa ridhaa ya kupigiwa kura Oktoba 28 atahakikisha anatenga maeneo ya malisho na majosho kwa ajili ya mifugo lengo ni kukabiliana na migogoro baina ya wafugaji na wakulima.

Mtega aliyasema hayo kwenye mkutano wa kampeni akiwa Kata ya Mapogoro, ambapo alisema miongoni mwa matatizo yanayowakabili wakazi wa Jimbo la Mbarali ni mapigano na migogoro kati ya wakulima na wafugaji wakigombania maeneo kwa ajili ya malisho na shughuli za kilimo.

Pia aliwaambia wananchi kuwa akipata ridhaa ya kuchaguliwa, atahakikisha anasimamia utoaji wa dawa za mifugo kwa wafugaji, ili kusaidia kukadhibiti na magonjwa ya mlipuko hasa kwa wanaohamahama, sambamba na kutatua tatizo la uhaba wa watumishi kwenye sekta ya kilimo na mifugo kwa kuishauri serikali kuongeza ajira.

"Wilaya yetu shughuli zake kuu ni kilimo cha mpunga na ufugaji, licha ya kubarikiwa maeneo makubwa kwa ajili ya kufanya shughuli hizo lakini bado kuna matatizo ambayo ni migogoro baina ya wakulima na wafugaji ambapo kila mmoja hutaka kutumia eneo la mwenzake kutokana na uoto uliopo kuvutia, nikipata ridhaa ya kuwaongoza Wanambarali mimi mbunge nitahakikisha tatizo hilo nalishughulikia kwa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya malisho ya mifugo na kilimo," alisema Mtega.

Alisema atakaa na jamii za wakulima na wafugaji kujua njia sahihi ya kuainisha maeneo yaliyosahihi kwa ajili ya ufugaji ili kuhakikisha pasiwapo mwingiliano wowote kama ilivyo sasa, ambapo huingiza mifugo kwenye mashamba ya mpunga.

Kuhusu suala la elimu msingi na sekondari, alisema ataandaa utaratibu wa kushindanisha viwango vya ufaulu kwa shule ili kuleta motisha na kwamba shule itakayofanya vizuri itapewa motisha ya fedha lengo likiwa ni kuongeza ufanisi na kiwango cha ufaulu kwa watoto wilayani humo.

"Kiu yetu ni kuona Wilaya ya Mbarali inafanya vizuri kwenye matokeo ya mitihani sio tu wilaya hii, bali mkoa wa Mbeya kwa ujumla ikumbukwe awali ufaulu ulikuwa kwa asilimia 67, lakini kutokana na bidii za viongozi na wadau mbalimbali mkoani humu, sasa tumefikia asilimia 85," alisema Mtega.



Mgombea udiwani viti maalum Kata ya Mapogoro, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Mariam Wakagunda, akiomba kura katika mkutano wa kampeni uliofanyika wilayani humo juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Polisi wakamata bunduki, bastola, risasi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limekamata silaha mbili zisizokuwa na namba zilizotengenezwa kienyeji bunduki aina ya Short Gun, bastola na risasi kumi kutoka kwa washukiwa wa uhalifu.

Walizikamata baada ya kuwashukia watu wanne waliokuwa kwenye pikipiki kuwa huenda ni wahalifu, ambao baada ya kuwaona askari walikimbia na kuzitelekeza silaha hizo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na kusainiwa na Kamanda wa Jeshi la Polisi, Ulrich Matei, tukio hilo lilitokea Oktoba 5, mwaka huu saa mbili usiku katika barabara ya Mbeya-Tabora katika Kijiji na Kata ya Mafyeko wilayani Chunya.

Alisema polisi wakiwa doria waliwatilia shaka watu wanne waliokuwa kwenye pikipiki ambao baada ya kuona gari la Polisi walishuka na kutelekeza pikipiki na begi dogo jeusi.

Aidha, katika upekuzi uliofanyika katika begi hilo, walikutwa bunduki mbili zilizotengenezwa kienyeji aina ya short gun na pistol, panga mbili, shoka moja iliyo na mpini na tochi mbili.

"Jeshi la Polisi linaendelea na msako wa kuwatafuta watuhumiwa hao na likifanikiwa kuwakamata watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma za kumiliki silaha kinyume na taratibu za nchi," alisema Matei.

Katika hatua nyingine, Jeshi la Polisi limesema mtu mmoja alipoteza maisha baada ya kuungua moto mwili mzima wakati akisafisha shamba lake huko katika Kijiji cha Sholongo Kata ya Swaya, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Mtu huyo aliyefahamika kwa jina la Hilda Kilela (66), mkazi wa "Airport" ya zamani aliungua moto Oktoba 5, mwaka juu majira ya saa sita mchana baada ya moto uliokuwa ukisafisha shamba kumzingira.

Jeshi hilo pia liliwaeleza waandishi wa habari kuwa limamshikilia Getruda Sheka (40), mkazi wa Kata ya Nzovwe kwa tuhuma za kuingiza vitenge doti 21 kutoka Malawi bila kulipia ushuru ambapo Oktoba 6, mwaka huu majira ya saa sita usiku.

Kutokana na matukio hayo, Kamanda Matei aliwaomba wananchi kuendelea kutoa taarifa wanapobaini uwapo wa matukio yanayohatarisha usalama wa raia na mali zao.

Alisema jitihada za kufanya misako, doria katika maeneo mbalimbali zinaendelea kuzaa matunda wamepunguza matukio ya uhalifu, ajali za barabarani na kukamata watuhumiwa wa matukio ya uhalifu.



# Dk. Mwinyi aahidi kuboresha ulinzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema endapo atapata ridhaa ya kuongoza Zanzibar, ataimarisha ulinzi na usalama katika sekta ya utalii ili watalii wanaofika Zanzibar wawe salama.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wawekezaji wa sekta ya utalii ikiwa ni mwendelezo wa kampeni zake za kukutana na makundi mbalimbali.

Dk. Mwinyi alisema Zanzibar sasa iko salama na wananchi wake wako salama, hivyo aliwahakikishia wawekezaji hao usalama unaendelea kuimarika, ili watalii waendelee kutembea katika vivutio mbalimbali vya Zanzibar.

Akizungumzia ucheleweshwaji wa maombi ya upatikanaji wa vibali vya kuishi pamoja na ufanyaji wa kazi, Dk. Mwinyi aliwahakikishia wawekezaji hao kuondoa urasimu wa aina zote.

Sambamba na hayo, alisema atahakikisha analisimamia suala la rushwa, ili wawekezaji kufanya kazi zao bila ya vikwazo.

"Naomba mniombee, nikichaguliwa kuwa rais wa Zanzibar, nitahakikisha kila kitu kinakaa sawa katika sekta hii ya utalii na kuzitatua kero zinazowakabili," alisema.

Kwa upande wao, wawekezaji hao walisema wamekuwa wakikabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwamo kuchelewa kupatiwa vibali vya uwekezaji na kumwomba mgombea huyo endapo atapata ridhaa, aliangalie suala hilo. Katika hatua nyingine, mgombea huyo alikutana na viongozi wa madhehebu mbalimbali ya dini ya Kikristo ambao walimweleza kuwapo kwa tatizo la ubaguzi.

Akizungumza katika kikao hicho, Askofu wa Kanisa la Katoliki, Jimbo la Zanzibar, Augustine Shayo, alisema hawataki upendeleo bali wanachokitaka haki itendeke hasa wanapopeleka kesi katika vyombo vya sheria.

"Matumaini yetu kwako kuwa na uongozi wa haki hatusemi kama tupendelewe, lakini tunataka haki itendeke kwa watu wote," alisema Askofu Shayo ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Wakristo Zanzibar.

Naye Dk. Mwinyi alisema katika uongozi wake atahakikisha anaondosha ubaguzi wa aina yoyote na kutoa haki sawa kwa wananchi wote.

"Kama upo ubaguzi hatupaswi kuufumbia macho, nikiingia madarakani nitahakikisha napambana na suala hili kwani nisipolifanyia kazi halitaondoka," alisema.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (katikati), akisalimiana na viongozi mbalimbali katika Shule ya Sekondari ya Fujoni, kabla ya kuweka jiwe la msingi katika ukumbi wa mitihani wa shule hiyo, Zanzibar jana. **PICHA: OMPR – ZNZ**

# Balozi Iddi asifu wananchi uibuaji miradi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema uamuzi wa jamii katika baadhi ya maeneo kusimamia wenyewe miundombinu ya miradi ya maendeleo ni jambo la msingi.

Amesema hatua hiyo inaakisi dhana nzima ya kupunguza gharama sambamba na kuepuka urasimu wa kucheleweshwa kwa wakati iliyopangwa.

Balozi Iddi alitoa kauli baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa ukumbi wa mitihani wa Shule ya Fujoni Mkoa wa Kaskazini Unguja. Ujenzi huo umeibuliwa na wananchi wa Kijiji cha Fujoni na kugharamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) .

Alisema iko mifano mingi ambayo wananchi wamekuwa wakishuhudia ya miradi wanayopewa kuitekeleza wahandisi wa kigeni, lakini matokeo yake huambatana na gharama kubwa zinazoweza kuepukwa na hatimaye kuibua miradi mingine mipya inayoweza kuwafaidisha wanajamii.

Baadhi ya wahandisi wa kigeni wanaokabidhiwa tenda za ujenzi wa miradi ya kijamii, alisema wanatabia ya ulaghai wakati wanapohitaji malipo ya kazi hizo na baadaye kuwa na sababu na visingizio visivyoisha katika kukamilisha miradi wanayokabidhiwa.

Balozi Iddi alisema tabia hiyo mbaya wakati mwingine huzorotesha kukamilika kwa wakati miradi na hatimaye kusababisha matatizo kwa wananchi, jambo linalokwenda kinyume cha mikataba iliyosainiwa kabla ya kuanza.

Kutokana na uibuliwaji wa miradi hiyo muhimu kwa ustawi wa jamii, Balozi Iddi aliwataka wanafunzi kujenga utamaduni wa kutunza rasilimali wanazojengewa ili zitumike na wanafunzi wa sasa na vizazi vijavyo.

Alisema serikali inawajibika kuwajengea mazingira bora watoto ili kukidhi vigezo vyao vya taaluma vinavyopaswa kwenda kwa kasi ya sasa ya sayansi na teknolojia.

Balozi Iddi aliitumia fursa hiyo kwa kuwahimiza wananchi kushiriki kwenye uchaguzi mkuu kwa amani na utulivu na kuwataka wazazi na wazee kuwaasa watoto wao kuepuka ushawishi wa baadhi ya wanasiasa walioshindwa kunadi sera zao na badala yake kuanza na viashiria vya vurugu.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa ukumbi huo, Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi, Ali Haji Abdullah, alisema wananchi wa Shehia ya Fujoni walitafakari na kuamua kuibua mradi huo ili kuwaondolea usumbufu watoto wao.

Alisema ujenzi wa jengo hilo la kisasa unakwenda sambamba na sera ya elimu ya kuwataka wanafunzi hasa wale wa sekondari na vyuo kufanya mitihani yao katika ukumbi mkubwa badala ya kutumia vyumba vya madarasa.

# ACT-Wazalendo yazoa wanachama 500

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA Cha ACT -Wazalendo jana, katika mkutano wake wa kampeni kilipokea wanachama wapya zaidi ya 500 na kukabidhiwa kadi za chama hicho.

Wanachama hao wapya walipokewa na mgombea wa urais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad, katika mkutano wa hadhara uliofanyika viwanja vya Kijini, Mkwajuni Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema wanachama hao wametoka CCM kwa sababu wameona ni vyema kuungana na Wazanzibar wengine ili waweze kujitawala wenyewe.

Maalim Seif alisema kuingia wanachama hao katika chama hicho kuwa ni dalili ya CCM kupoteza dira na mwelekeo katika siasa za Zanzibar na kuwataka wajiandae kisaikolojia kuondoka madarakani.

Sambamba na hilo alisema wanachama wengi wa CCM wanatoka huko kwa sababu wanataka kuona Zanzibar yao ikiwa na mamlaka kamili.

Maalim Seif alisema akiwa Rais wa Zanzibar atahakikisha migogoro ya ardhi inamalizika katika visiwa vya Zanzibar.

Aliwaomba wananchi wa mkoa huo kumchagua yeye na baada ya kumchagua atahakikisha kila aliyenyang'anywa ardhi atarudishiwa.

Mgombea huyo alisema kama kuna mtu amejenga katika ardhi ambayo alipora, atatakiwa kutoa fidia ya kipindi chochote ambacho anatumia ardhi hiyo.

"Wananchi wengi wamenyang'anywa ardhi zao kwa sababu tu mtu yuko katika madaraka, lakini tukiingia Ikulu tu watu waliojenga katika ardhi za watu watalipa fidia mara moja," alisema Maalim Seif.

Alisema wako baadhi ya viongozi kazi yao kuwadhulumu wananchi ardhi kwa sababu wana mamlaka katika utawala na kueleza kuwa akiingia madarakani lazima zifuatiliewe kwa haraka sana.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Nipashe

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0782253676

Nipashe

## KUPOTEA KWA CHETI



**BAZIR NDEGE** Anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2354/0010** kilichotolewa na Baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **EAGLES** mwaka 2011, yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi . Taarifa ya polisi **DAR/OST/RB/715176/2020**

115934702

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**INFLIGHT CATERING SERVICES LIMITED**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA HILUX YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 518 ARF.** CHASSIS NAMBA **LN850023424.** ENGINE NAMBA **2L2168623.** YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/JNI/RB/675742/2020.**

115933202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA SHERIA**

**IDARA YA MAHAKAM**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA2.**

**Katika mahakama ya mwanzo ya KINONDONI**

**usimamizi wa mirathi 169/2020**

**Ombi la CAROLINE KILIWA na WILFRED KILIWA msimamizi wa mirathi ya marehemu EUGENE KILIWA.**

Watu wote wanaohusika na usimamiziwa mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria Mahakamani kesi wakati wa kusikiizwa kesi mnamo tarehe 30/10/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hii.
Wosia wa marehemu upo mahakamani waweza kukaguliwa.

115933102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA: 278...2020**

**Mdai: MENGI LUSEGA LUBUWA**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa: (1) RICHARD MSHANDETE (2) ENOCK LATA**

Kwa: (1) **RICHARD MSHANDETE**
**FOREST - BOMA**
(2) **ENOCK LATA**
**MALINYI-MAHENGE**

**Ombi la Mdai: MENGI LUSEGA LUBUWA**

**Madai ya: PESA Sh. LAKI TANO NA ELFU HAMSINI (550,000).**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 20 mwezi 10 mwaka 2020 saa 02:30 Asubuhi.
Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 06 mwezi 10 mwaka 2020.

MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

115933802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;300/2020**

**Ombi la SHAKILA JUMA MLANZI,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu JUMA HALFAN MLANZI.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 10/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 06/10/2020.

Tarehe 06/10/2020

115933702

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Antidius M. Aloys**
amepotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 271 AEN.** Ametoa taarifa polisi na kupewa RB Number **KAG/BUK/RB/697456/2020.** Kwa yeyote atakayeipata atoe taarifa polisi na awasiliane naye kwa namba **0765665660.**

115935802

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RUKIA IRENE MNZAVA**
anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA RUSH** yenye namba ya usajiri **T630 DED** , iliyotolewa na mamlaka ya mapato Tanzania .
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Polisi Taarifa **KW/RB/4965/2020**

115935402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;301/2020**

**Ombi la MARIAM WILLIAM NYANGE ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu WILLIAM EDWARD NYANGE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 07/10/2020.

Tarehe 7/10/2020

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115935102

**IN THE DISTRICT COURT OF GEITA**
**AT GEITA**

**MISC/CIVIL/APPLICATION CASE NO. 10 OF 2020**

**EMMANUEL PASCHAL MSHAN GA.............APPLICANT**

**VERSUS**

1. **FERRANT PROCESSING COMPANY LTD.................DEFENDANT/RESPONDENT**
2. **NYARUGUSU MINE CO. LTD**
3. **BORASSUS CO. LTD**

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**

**TAKE NOTICE THAT,** the above case has been fixed for mention on the 8 day of October, 2020 at 8.30am in the forenoon. YOU ARE required to appear in this court without fail and you must produce on that day all document upon which you intend to rely in support of your case.
**GIVEN UNDER** my hand and the SEAL of the Court this 24 day of September, 2020.

115933902

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Marais wanne wa Afrika wajadili usalama Congo

**KINSHASA, Congo**

MARAIS wa nchi nne za Kanda ya Maziwa Makuu jana wamejadili masuala ya kiusalama ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na nchi jirani.

Viongozi hao walijadili kwenye mkutano wa kilele wa siku moja ambao uliitishwa na Rais wa Congo, Felix Tshisekedi na kuendeshwa kwa njia ya video.

Hata hivyo, Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye, hatohudhuria mkutano huo.

Mwenyeji wa mkutano huo, Rais Felix Tshisekedi aliutumia kuwashawishi marais wenzake, Paul Kagame wa Rwanda, Yoweri Museveni wa Uganda na Joao Lourenco wa Angola kuhusu jitihada za pamoja kwa ajili ya usalama hasa katika majimbo ya Kivu ya Kaskazini, Kivu ya Kusini na Ituri.

Wataalamu na mawaziri wa mambo ya nje walijadili ajenda ya mkutano huo kabla ya kikao hicho cha marais hao.

Awali, Waziri wa Mambo ya Nje wa Congo, Marie Nzeza alisema kwamba marais hao watajadili pia kuhusu janga la virusi vya Corona, masuala ya kibiashara na uhusiano bora.

"Sababu ya mkutano huu wa kilele uliotishwa na Rais Tshisekedi, ni kuwako na tathmini ya kina ya viongozi wa Rwanda, Uganda, Angola, Kongo na Burundi, kuhusu hali kwa ujumla kwenye kanda hiyo na hasa ustawi wake."

***DW***



Miongoni mwa nyumba iliyokumbwa na mafuriko. **PICHA: MTANDAO**

## Mamilioni wakumbwa na mafuriko

**WASHINGTON, Marekani**

TAKWIMU za Umoja wa Mataifa (UN), zinaonyesha idadi ya watu waliokumbwa na mafuriko yatokanayo na mvua za msimu Afrika Mashariki imeongezeka mara tano zaidi katika kipindi cha miaka minne.

Karibu watu milioni sita wameathirika mwaka huu huku milioni 1.5 kati yao wamelazimika kuyaacha makazi yao.

Sehemu ya ukanda huo imerekodi mvua kubwa kuwahi kutokea katika kipindi cha karne moja.

Mwaka 2019, tofauti kubwa ya joto kati ya pande za Mashariki na Magharibi mwa Bahari ya Hindi ndiyo ilikuwa sababu ya kuwapo kwa mvua kubwa.

Takwimu zilizokusanywa na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Uratibu wa Masuala ya Kibinadamu zinatoa picha ya kutia wasiwasi, anaripoti Catherine Byaruhanga wa BBC.

Idadi ya walioathiriwa na mafuriko Afrika Mashariki imetoka watu milioni 1.1 mwaka 2016 hadi milioni nne mwaka jana na sasa karibu watu milioni sita.

Hii ni kabla ya mvua fupi, ambazo kawaida huongezeka mwezi Novemba na kuathiri nchi nyingi katika ukanda.

Sudan ni moja ya nchi zilizoathirika zaidi, nyumba za watu 860,000 zimeharibiwa na zaidi ya watu 120 wamepoteza maisha, UN ilisema ikinukuu takwimu za serikali.

Karibu kila jimbo nchini humo limekumbwa na mafuriko makubwa na katika nchi jirani ya Sudan Kusini, watu 800,000 wameathirika na watu 368,000 wakilazimishwa kuyaacha makazi yao.

**BBC**

# Mpango wa makombora Korea Kaskazini ni tishio

**PYONGYANG, Korea Kaskazini**

KOREA Kaskazini inaaminika kuwa na makombora yenye uwezo wa kupiga maeneo ya masafa marefu, ikiwamo Marekani.

Inadai kuwa imetengeneza bomu la haidrojeni na kuliweka kwenye kombora.

Hivi karibuni, uhusiano na Marekani na Korea Kusini ulishuka, baada ya Pyongyang kulipua ofisi ya uhusiano wa Kaskazini-Kusini katika eneo la mpaka.

Katika kipindi cha mwaka 2017, Korea Kaskazini ilijaribu makombora kadhaa kuonyesha maendeleo ya haraka ya teknolojia yake ya kijeshi.

Hwasong-12 ilifikiriwa kuwa inaweza kufikia umbali wa kilomita 4,500 (maili 2,800), ikiiweka ngome ya jeshi la Marekani kwenye kisiwa cha Pacific cha Guam katika umbali mzuri wa kuipiga.

Baadaye, Hwasong-14 ilionesha uwezo mkubwa zaidi huku tafiti nyingine zikionesha kwamba inaweza kusafiri hadi kilomita 10,000 ikiwa itarushwa anga za juu.

Hii ingeipa Pyongyang kombora lake la kwanza (ICBM), linaloweza kufikia New York. Hatimaye, Hwasong-15 ilijaribiwa, ikifika umbali wa wastani wa kilomita 4,500 mara 10 zaidi kuliko Kituo cha Anga cha Kimataifa.

Kombora likiwa limefyatuliwa linaweza kusafiri kwa umbali wa kilomita 13,000, na kuiweka kwenye shabaha eneo la bara la nchi ya Marekani.

Hata hivyo, mashaka yanabaki ikiwa makombora haya yanaweza kufanikiwa kubeba silaha ya vita kwa umbali kama huo, na ikiwa Korea Kaskazini ina utaalamu wa kufikia lengo. Mwaka 2019, Korea Kaskazini ilifanya majaribio kadhaa ya kombora la masafa mafupi, ambayo iliongezeka mwezi Julai na Agosti kwa kile ilichokiita maonyo kwa Marekani na Korea Kusini kuhusu mazoezi yao ya kijeshi

Mwezi Oktoba, Pyongyang ilionekana kuwa na uwezo mpya ilipojaribu kombora linaloweza kurusha kutoka kwenye nyambizi.

Kuzindua kombora lenye vifaa vya nyuklia kutoka kwenye nyambizi imeongeza uwezo wa Korea Kaskazini wa kushambulia.

Tishio hilo linakabiliwa na meli za zamani na ndogo za nyambizi za nchi hiyo, ambazo zinaweza kufanya safari ya kwenda moja kwa moja hadi Hawaii.

Mafanikio dhahiri ya majaribio haya yote yameibua maswali kuhusu namna ya mpango wa makombora wa Korea Kaskazini ulivyoimarika haraka.

Waangalizi wanaamini Pyongyang inaweza kuwa imepata injini zinazofanya kazi kwa kiwango cha juu kutoka kwa mitandao haramu nchini Urusi na Ukraine.

***BBC***



# KEPA:

## SINA WASIWASI NA NAFASI YANGU CHELSEA

**LONDON, England**

KIPA wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga, amesema kupoteza nafasi kwenye kikosi cha kwanza hakutammaliza, kwani ndio kutamjenga na atarudi kwenye nafasi yake muda si mrefu.

Mlinda mlango huyo raia wa Hispania mwenye umri wa miaka 26, ambaye ndiye kipa ghali zaidi duniani, alijiunga na Chelsea mwaka 2018 akitokea Athletic Bilbao kwa ada ya pauni milioni 71.

Lakini mapungufu ya msimu uliopita na machache msimu huu yamemfanya apoteze namba kwenye kikosi cha kwanza pale kwenye dimba la Stamford Bridge.

"Katika maisha ya soka kuna nyakati za kupanda na kushuka," alisema Kepa akinukuliwa na Sky Sport.

"Lakini hatima yake ni kufanya kazi kwa bidii zaidi, hilo ndilo ninaloweza kulifanya kwa sasa."

Kepa, ameshushwa nafasi na kocha wake Frank Lampard na kumpa nafasi kipa mpya, kama chaguo lake la kwanza.

Itakumbukwa mechi ya Liverpool ilimsababishia kuwekwa kando na kuanza kutumiwa Willy Caballero mwenye umri wa miaka 39, jambo lililowafanya Chelsea kuingia sokoni kusaka mbadala wake, ambaye ni Edouard Mendy mwenye umri wa miaka 28.

Mlinda mlango huyo wa kimataifa wa Senegal, Mendy tayari katika mechi za awali, ambazo amecheza akiwa Chelsea ameonyesha uwezo mkubwa na kusahihisha makosa yaliyokuwa yanajitokeza kwa Kepa, lakini bado Kepa anaamini atarudi kwa nguvu zaidi.

## SANCHO AITIBUA DORTMUND

**DORTMUND, Ujerumani**

KLABU ya Borussia Dortmund imekasirishwa na kitendo cha staa wao, Jadon Sancho kwenda kwenye sherehe ya Tammy Abraham.

Nyota huyo aliyekuwa akisakwa na Manchester United kwa muda wote wa dirisha la uhamisho, ambaye kwa sasa yupo kwenye kikosi cha England, alikosekana kwenye mechi ya Dortmund iliposhinda 4-0, dhidi ya Freiburg huku yeye akiripotiwa kuwa mgonjwa.

Jambo hilo lilimfanya akosekane mazoezini tangu mwanzoni



mwa wiki iliyopita, lakini ripoti zinadai Sancho alikuwa mmoja wa mastaa watatu wa England, ambao walikwenda kwenye sherehe ya Abraham ya kutimiza umri wa miaka 23.


Sancho, Abraham na Ben Chilwell walikuwa sehemu ya sherehe hiyo iliyokuwa na wageni 20, marafiki na wanafamilia.

Wote hao wanatarajia kucheza dhidi ya Wales, Alhamisi hii huku kitendo hicho kikiwaweka kwenye hatari kubwa ya kupigwa chini.

Mmoja wa maofisa wa klabu ya Dortmund, ambaye hakuweka wazi jina lake amenukuliwa akisema, "Sancho amekosa weledi kama mchezaji mkubwa, na anaweza kuadhibiwa."

Hata hivyo, klabu hiyo bado haijatoa tamko lolote, huku Sancho mwenyewe akinukuliwa kuomba radhi kwa kitendo hicho.

## Klopp: Liverpool bado ni imara



**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amesema licha ya Liverpool kufungwa kwenye mchezo wa Ligi Kuu, lakini kikosi chake bado kipo imara.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu England walikumbana na kipigo kizito huko Villa Park walipochapwa mabao 7-2 na Aston Villa, huku straika Ollie Watkins akipiga hat-trick.

Jambo hilo limekuja baada ya Jumatatu iliyopita, kocha huyo kurushiana maneno na gwiji wa Manchester United, Roy Keane alipohoji uwezo wa kukaba wa timu hiyo kwenye ushindi wao wa 3-1 dhidi ya Arsenal.

"Tumekosea tu mchezoni baada ya kuwa nyuma kwa 1-0, lakini hakiwezi kuwa kisingizio. Unaweza kuwa nyuma kwa bao 1-0 na unafanya mambo unayotaka," alisema Klopp akinukuliwa na tovuti ya klabu hiyo.

"Ukabaji wetu ulikuwa wa kawaida sana na hatuweza kurudi kwenye mchezo, kila kitu kilikataa. Tulifanya makosa mengi sana na makubwa. Ilianzia kwenye goli la kwanza na tuliendelea kufanya makosa mengine.

"Haya makosa yote yametokea kwenye mechi moja. Si kwamba timu yetu ni mbovu kama bwana Keane alivyosema."



# MANCINI

## ASIKITIKA EMERSON KUBAKI TENA CHELSEA

**FLORENCE, Italia**

KOCHA mkuu wa timu ya Taifa ya Italia, Roberto Mancini, amebainisha kwamba alikuwa na matumaini ya Emerson Palmieri angeweza kuondoka Chelsea wakati wa dirisha la usajili, ili apate sehemu ya kucheza mara kwa mara.

Mlinzi huyo wa kushoto amekuwa hana nafasi ya kucheza kwa kipindi cha miaka miwili na nusu aliyokaa pale Stamford Bridge na alikuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Ligi Kuu Italia, Serie A.

Juventus waliripotiwa kuwania zaidi kumsajili Emerson mwenye umri wa miaka 26, katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili pamoja na klabu yake ya zamani ya Roma.

Hata hivyo, usajili huo haukufanikiwa na sasa anaonekana atabakia jijini London, ingawa dirisha la usajili bado halijafungwa nchini Ureno kwa wiki moja zaidi.

Mancini ameonyesha kusikitishwa kwake na Emerson kushindwa kupata klabu mpya, ili aweze kuwa na muda wa kucheza mara kwa mara.

Emerson yupo kwenye kikosi cha Italia kinachojiandaa kucheza mchezo wa kirafiki na Moldova na ule wa Ligi ya Mataifa ya UEFA dhidi ya Uholanzi.

"Nilikuwa natumaini Emerson angeweza kupata timu mpya, ili acheza mara kwa mara," alisema Mancini akiwaambia waandishi wa habari jana Jumatano kabla ya kuivaa Moldova mjini Florence.

"Alipaswa kuondoka, ili akapate changamoto sehemu nyingine ambako atacheza mara kwa mara."



## GIROUD: KUKOSEKANA KWA BENZEMA UFARANSA NI AIBU

**PARIS, Ufaransa**

KUKOSEKANA kwa Karim Benzema kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Ufaransa ni "aibu" na ni kama "tatizo", lakini Olivier Giroud amesisitiza hana cha kufanya zaidi ya kumheshimu tu straika mwenzake huyo.

Mshambuliaji huyo wa Real Madrid, Benzema hajaichezea timu ya Taifa ya Ufaransa tangu mwaka 2015 akiwekwa pembeni kutokana na kuhusika katika mgogoro na Mathieu Valbuena.

Giroud amejiimarisha yeye mwenyewe kama mchezaji muhimu wa kikosi cha Ufaransa kwenye safu ya ushambuliaji na jana Jumatano alitarajia kucheza mechi yake ya 100 ya kimataifa kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Ukraine.

Tangu kuachwa kwa Benzema kumekuwa na shutuma nyingi kwa uwapo wa Giroud kwenye kikosi hicho cha 'Les Bleus'.

Alipoulizwa kuhusu kufananishwa kwake na straika huyo wa Chelsea kwenye mtandao wa kijamii Aprili mwaka huu, Benzema alijibu: "Usifananishe mbio za magari ya F1 na vitoroli... na anajua kwamba mimi ni F1."

Lakini Giroud alisisitiza hana tatizo lolote na mchezaji huyo wa zamani wa Lyon.

"Kiukweli kabisa ni aibu, kwa sababu Karim anabaki kuwa mchezaji muhimu na mwenye ubora wake," alisema Giroud akiiambia RMC.

"Mimi binafsi sina tatizo lolote na yeye, historia ilitaka sisi kuwa wapinzani. Mara zote nimekuwa namwelewa na namuheshimu."

## GOTZE AJIUNGA NA PSV

**AMSTERDAM, Uholanzi**

MARIO Gotze amejiunga na miamba wa Ligi Kuu ya Uholanzi, PSV baada ya kuachwa na Borussia Dortmund.


Mchezaji huyo wa zamani wa Bayern Munich, ambaye ameichezea Ujerumani mechi 63, amesaini mkataba wa miaka miwili na klabu hiyo ya Eindhoven.

Gotze, ambaye alifunga bao la ushindi kwenye Kombe la Dunia mwaka 2014 na kuwafanya Ujerumani kulitwaa kombe hilo, kwa sasa ana umri wa miaka 28 na amekuwa na wakati mgumu wa ufiti wake katika miaka ya hivi karibuni.

Gotze alicheza mechi 21 tu kwa Dortmund msimu wa 2019-20 na amesema alikuwa na ofa nyingi kabla ya kwenda Uholanzi.

Alipoulizwa kuhusu uhamisho wake huo, Gotze alisema: "Nilikuwa naendelea kufanya mazoezi ili niwe fiti.

"Kwa sasa nasubiri kuitumikia timu yangu mpya na kukutana na wachezaji wapya kwa ajili ya mechi zinazokuja."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GIGGS AMUONYA CAVANI MAN UTD

Wachezaji wa Amerika Kusini wamekuwa na wakati mgumu United baada ya Falcao, Di Maria, Sanchez kuboronga, huku...

**MANCHESTER, Englend**

RYAN Giggs amempa onyo straika mpya wa Manchester United, Edinson Cavani kuwa anatakiwa kupambana, ili kuweza kung'ara katika klabu hiyo.

Cavani ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Uruguay mwenye umri wa miaka 33, alikamilisha uhamisho wa kutua Man United siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili, Jumatatu usiku.

Alitua Man United kwa uhamisho huru baada ya kumaliza mkataba wake kule kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Paris Saint-Germain.

Amesaini mkataba wa mwaka mmoja na kupewa kipengele cha kuongezewa miezi 12.

Hata hivyo, gwiji wa Man United, Giggs amesema, Cavani atahitaji kuwa na muda kidogo kabla ya kuanza kuendana na kasi ya kikosi hicho cha kocha Ole Gunnar Solskjaer.

"Cavani hatakuwa na shida ya ukubwa wa klabu. Ni mchezaji wa kiwango cha daraja la juu, nadhani uzoefu wake utamsaidia," alisema Giggs akinukuliwa na Sky Sport.

"Macho ya watu yataelekezwa kwake na atalazimika kufanya kweli kwa sababu presha itakuwa kwake.

"Nadhani Man United inahitaji mshambuliaji wa kati. Wanahitaji mtu wa hivyo kuwafungia mabao. Bila ya shaka atalifanya hilo."

"Wasiwasi wa Giggs unakuja sehemu moja tu kwamba wachezaji wengi wa kutoka Amerika Kusini wamekuwa na wakati mgumu wanapotua kwenye kikosi cha Man United baada ya Radamel Falcao, Angel di Maria na Alexis Sanchez kuboronga.

## KWA UFUPI

**UTD YAJITETEA KWA SANCHO**
MANCHESTER United iliamua kuachana na mango kwa kumsajili mshambuliaji, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20, baada ya kufanya mahesabu na kugundua wangetumia kiasi cha pauni milioni 227, kwa sababu ya ada yake ya pauni milioni 108 pamoja na mshahara na ada ya wakala wake. ***(Guardian)***

**SHAQIRI WA3 CORONA LIVER**
XHERDAN Shaqiri anakuwa mchezaji wa tatu Liverpool kukutwa na virusi vya corona zaidi ya wiki moja iliyopita, wengine ni Thiago Alcantara, ambaye amejiunga na timu hiyo akitokea Bayern Munich, pamoja na Sadio Mane. ***(LiveScore)***

**WEST HAM WAMKOSA TOMORI**
WEST Ham walikuwa wanataka kumsajili mlinzi wa England, Fikayo Tomori mwenye umri wa miaka 22, kwa mkopo na walimpa ofa ya kumlipa mshahara wa pauni 50,000 kwa wiki, lakini dili hilo lilishindikana. ***(Talksport)***

**RODON LULU SPURS, WEST HAM**
KLABU ya Tottenham na West Ham zinamwania mlinzi wa kati wa Swansea raia wa Wales, Joe Rodon mwenye umri wa miaka 22, na zinaweza kutoa ofa ya pauni milioni 1. ***(Wales Online)***

**WIJNALDUM AIKATALIA BARCA**
KIUNGO wa Liverpool na Uholanzi, Georginio Wijnaldum alikataa ofa ya kwenda kujiunga na Barcelona. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, mkataba wake pale Anfield unamalizika kipindi kijacho cha majira ya joto. ***(Mirror)***

**ARSENAL, ETIENNE ZATOFAUTIANA**
KLABU ya Ufaransa ya Saint-Etienne imeishutumu Arsenal kwa kushindwa kuruhusu mlinzi, William Saliba mwenye umri wa miaka 19, kurudi katika klabu yake. ***(Talksport)***

**BARCA KUMSAJILI GRACIA**
BARCELONA itasubiri hadi kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2021, ili kumsajili mlinzi wa Hispania, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 19, kutoka Manchester City. Ofa ya Barca ya euro milioni mbili ilikataliwa na City siku ya mwisho ya kufungwa kwa pazia la usajili. ***(Marca)***

**DEMBELE AMTIBULIA DEPAY**
MPANGO wa Barcelona kutaka kumsajili nyota wa Lyon na timu ya Taifa ya Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 26, ulishindikana baada ya Ousmane Dembele mwenye miaka 23, kukataa kwenda Manchester United. ***(AS)***

**CHELSEA YAMNASA TLEMCANI**
CHELSEA imemsajili kipa kinda wa miaka 16, Sami Tlemcani, kutoka klabu inayoshiriki Ligue 2, Paris ya Ufaransa. ***(LiveScore)***

**RAHMAN AWANIWA WATFORD**
KLABU za Watford na Middlesbrough zinawania kumsajili mlinzi wa kushoto wa Chelsea na Ghana, Baba Rahman mwenye umri wa miaka 26 kwa mkopo wa muda mrefu. ***(Goal)***

**MOWATT APATA OFA KIBAO**
KLABU za Middlesbrough, QPR na Cardiff City zinamwania kwa karibu mlinzi wa kati wa Barnsley, Alex Mowatt mwenye umri wa miaka 25. ***(Football League World)***

**DAWSON KIDUCHU WEST HAM**
WEST Ham wangeweza kukamilisha usajili wa mlinzi wa Watford, Craig Dawson mwenye umri wa miaka 30, lakini walihitajika kulipa pauni milioni 4. ***(Sun)***

**WATFORD YAMWEKEA NGUMU SARR**
OMBI la Manchester United la kutaka kumsajili winga wa Watford, Ismaila Sarr mwenye umri wa miaka 22 kwa mkopo wa muda mrefu, lilikataliwa kwani walikuwa wanataka kumuuza moja kwa moja. ***(Manchester Evening News)***

HABARI MICHEZO

# CHAMA AFUNGUKA MADAI MICHO KUMTEMA ZAMBIA

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO nyota wa Klabu ya Simba, Claotus Chama, amefunguka kuhusu kauli ya Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Zambia, Milutin Sredojevic 'Micho', aliyoitoa akidai mchezaji huyo na mwenzake, Rally Bwalya pamoja na Obrey Chirwa wa Azam FC ni watovu wa nidhamu.

Micho alitoa kauli hiyo baada ya wachezaji hao kuchelewa ndege ya kusafiri kwenda kujiunga na wenzake katika kambi ya timu ya Taifa ya Zambia 'Chipolopolo' kwa ajili mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Kenya, Harambee Stars itakayopigwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Kasarani jijini Nairobi.

Chama ameamua kuandika kwenye mtandao wake wa kijamii ujumbe mrefu kuhusiana na tukio hilo, baada ya Micho, kumtema kwenye kikosi cha timu hiyo, akiwa na wachezaji wenzake Wazmbia wanaocheza Ligi Kuu ya Tanzania, Bwalya na Chirwa.

Micho alidai kuwa wachezaji hao ni watovu wa nidhamu kwani wameshindwa kuungana na wenzao kama walivyotakiwa baada ya kuachwa na ndege mara mbili, huku kukiwa na mchezaji aliyesafiri kutoka nchini Urusi, kilometa 10,000, lakini amewahi kufika.

Katika ujumbe wake mrefu, Chama alisema kwanza ana maelewano mazuri na kocha huyo, lakini na Shirikisho la Soka nchini Zambia. Hata hivyo, alisema hakuchelewa ndege mara mbili kwa makusudi kama ilivyoelezwa, bali haikuwa rahisi kusafiri na ndege ya kwanza kwa sababu ilitakiwa asafiri Jumatatu saa 3:00 asubuhi wakati jana yake alikuwa amecheza mechi ya ligi jijini Dodoma iliyomalizika saa 12:00 jioni.

"Haikuwa rahisi kusafiri na ndege ya kwanza kwa sababu ilikuwa ni Jumatatu saa 3:00 asubuhi wakati mechi yetu (Simba dhidi ya JKT Tanzania), ilimalizika Jumapili jioni Dodoma na ni ngumu kutoka huko kurejea Dar es Salaam kwa sababu ni takriban mwendo wa saa nane kwa basi, lakini timu yake ya Simba haikuwa na mpango wa kusafiri haraka baada ya mchezo kumalizika," alisema.

Akaendelea kuandika: "Tiketi ya pili ilikuwa ni Jumanne saa 2:45 asubuhi, lakini wakati najiandaa nikaambiwa sikutakiwa kusafiri majira hayo ya asubuhi."

Chama alisema hakubaliani na Wazambia wengi wanaoamini kuwa hana nidhamu, lakini ukweli ni kwamba hakukosa ndege hizo kwa makusudi, lakini mwisho akaitakia timu yake ya Chipolopolo na Wazambia wote mafanikio kwenye mechi yao.




Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Tully Mwambapa (wa pili kulia), akijaribu kufunga katika hafla ya kutangaza udhamini wa Sh. milioni 200 kwa Ligi ya Mpira wa Kikapu ya Taifa 2020 (CRDB Bank Taifa Cup) iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Ligi hiyo inatarajiwa kufanyika jijini Dodoma katika viwanja vya Chinangali kuanzia Novemba 12-21, mwaka huu. Wengine pichani, kushoto ni Katibu Mkuu wa Shirikisho la Mpira wa Kikapu nchini(TBF), Mike Mwita, Msimamizi wa Vipindi vya Michezo Azam TV, Michael Maluwe na kulia ni Ofisa Uendeshaji Mkuu wa Kampuni ya Sanlam, Geofrey Masige. **MPIGAPICHA WETU**

# CRDB yadhamini Ligi ya Taifa ya Kikapu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Ligi ya Taifa ya Mpira wa Kikapu ikitarajiwa kuanza kutimua vumbi jijini Dodoma katika viwanja vya Chinangali kuanzia Novemba 12 kabla ya bingwa wa ligi hiyo, kujulikana Novemba 21, mwaka huu, Benki ya CRDB imeongeza utamu baada ya kutangaza kuidhamini kwa Sh. milioni 200.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Mawasiliano wa CRDB, Tully Mwambapa, alisema benki hiyo imefikia makubaliano na Shirikisho la Mpira wa Kikapu nchini (TBF) ya udhamini wa ligi hiyo ya taifa ya mpira wa kikapu ambayo imepewa jina la "CRDB Bank Taifa Cup".

Mwambapa alisema udhamini wa ligi hiyo ni mwendelezo wa jitihada za CRDB katika kuwawezesha vijana wa Kitanzania kupitia michezo na kwamba benki hiyo kupitia sera yake ya Uwezeshaji katika Jamii (CSI Policy) imekuwa ikiwekeza katika michezo ya vijana kwa kuamini kuwa inasaidia kuongeza ushiriki wao katika shughuli mbalimbali za maendeleo katika jamii.

Akizungumzia kuhusu msukumo uliosababisha benki hiyo kudhamini ligi hiyo yenye kauli mbiu ya "Ni Zaidi ya Game, Ni Maisha", Mwambapa alisema mchezo wa mpira wa kikapu umekuwa haupewi sana kipaumbele ukilinganisha na michezo mingine, hivyo kuwakatisha tamaa vijana wengi ambao wamekuwa wakionyesha vipaji katika mchezo huo.

"CRDB Bank Taifa Cup" inakuja kuleta hamasa si tu kwa vijana na wapenzi wa mpira wa kikapu bali kwa Watanzania wote kwa kuwaonyesha umuhimu wa kuwekeza katika michezo ya vijana na fursa zilizopo ikiwamo ajira," alisema Mwambapa.

Mwambapa alisema mbali na zawadi zitakazokuwa zikitolewa kwa timu zitakazofanya vizuri katika "CRDB Bank Taifa Cup", Benki ya CRDB pia imetenga kiasi cha Sh. milioni 50 kwa ajili ya "Scholarship" (ufadhili) kwa wachezaji watakaofanya vizuri.

"Tutakuwa pia na zawadi kwa ajili ya wapenzi wa mpira wa kikapu katika kila hatua za mashindano. Niwaombe Watanzania waanze kutufuatilia kupitia Azam TV na mitandao yetu ya kijamii kujua namna ya kushiriki," aliongezea Mwambapa.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania, Mike Mwita, aliishukuru Benki ya CRDB kwa kudhamini ligi hiyo, huku akieleza udhamini huo utaongeza mapenzi ya mpira wa kikapu kwa vijana kama ilivyo kwa mpira wa miguu na michezo mingine.

Mwita alisema: "Tunafurahi sana kwa udhamini na ushiriki thabiti wa Benki ya CRDB katika jitihada hizi zinazolenga kukuzwa kwa mpira wa kikapu nchini. Sio tu kwamba udhamini wa Benki ya CRDB utaboresha kiwango cha ligi, lakini utavutia Watanzania wengi kufuatilia mchezo huu na kuhamasisha vijana wengi kushiriki. "

## Mechi tano makocha wawili waaga Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA ni mwezi mmoja tu baada ya Ligi Kuu ya Tanzania Bara kuanza, tayari makocha wawili wa klabu zinazoshirki ligi hiyo wametimuliwa ambao ni Zlatko Krmpotick wa Yanga na Maka Malwisi wa Ihefu.

Wakati Kocha wa Yanga ni Mserbia, Maka ni Mtanzania na wote wametimuliwa, ndani ya mwezi mmoja tu tangu kuanza kwa ligi hiyo Septemba 6, mwaka huu na mpaka ilipofika juzi Oktoba 6, tayari wote wawili walikuwa wameshafungashiwa virago vyao.

Hata hivyo, makocha hao wametimuliwa kwa sababu tofauti. Ingawa viongozi wa Yanga hawakuweka wazi sababu halisi ya kumtimua, lakini habari za ndani zinaeleza kuwa ameshindwa kuiunganisha timu na kucheza soka la kuvuti kwa muda uliotakiwa.

Pamoja hayo, kocha wa Yanga ametimuliwa akiwa ameiongoza timu hiyo kwenye mechi tano, ikishinda nne na kutoka sare moja kwenye mechi za Ligi Kuu, akiiacha ikiwa na nafasi ya tatu kwa pointi 13.

Kwa upande wa Maka, klabu ya Ihefu juzi ilitoa taarifa rasmi ya kusitisha mkataba na kocha huyo aliyeipandisha Ligi Kuu, huku Bodi ya Wakurugenzi ikieleza kuwa inamtakia kila la kheri kocha huyo kwenye maisha mengine ya soka.

Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo Zagalo Chalamila alisema wameachana na kocha huyo kutokana na matokeo mabovu.

"Ni kwa sababu ya matokeo mabovu ambayo tumekuwa tunayapata. Kama unavyojua, Bodi ilibidi ikae haraka kwa sababu hakuna muda wa kusubiri, timu zinashuka nne, na mbili zinakwenda kucheza mechi za mchujo, kwa hiyo ilibidi tutoke na maazimio hayo kwa manufaa ya klabu yetu," alisema Chalamila, wakati huu Ihefu ikiwa imecheza mechi tano, ikishinda moja na kufungwa nne, na nafasi ya 17 na pointi zake tatu.

## BASATA kuwasaidia wasanii mikataba

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

BARAZA la Sanaa Tanzania (Basata), limewataka wasanii kuwa makini wakati wa kujaza mikataba yao na mapromota kwa kuwashirikisha wataalamu hatua itakayowawezesha kupata haki zao stahiki.


Hayo yamebainishwa na Katibu Mtendaji wa Basata, Godfrey Mngereza, wakati wa warsha ya siku moja ya kuboresha mahusiano kati ya waandishi na Basata.

Waandishi hao wanaoandika habari za sanaa za utamaduni pia ni wanachama wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Mwanza, MPC .

Mngereza alisema kila mahali sanaa zipo na kwamba ili kuondokana na changamoto hiyo na kuleta nuru na mafanikio kwa wasanii, huduma hiyo inatolewa na Basata bure, hivyo waitumie fursa hiyo ipasavyo kwa kuwa ofisi yake na maafisa wake wapo tayari kufanya kazi na wadau wa sanaa kwa muda wote.

Aliongeza kuwa Basata ina jukumu kubwa la kufufua na kukuza maendeleo ya sanaa nchini, uzalishaji wa kazi za sanaa pamoja na kuhakiki ushiriki wa jamii katika kazi za sanaa na wanafanya kazi kwa karibu zaidi na COSOTA, Bodi ya Filamu nchini, BAKITA na TCRA kwa lengo la kuhakikisha kazi za wasanii zinalindwa.

Michezo
Alhamisi Oktoba 8, 2020
Nipashe



GIGGS AMUONYA CAVANI MAN UTD

HABARI UK 22

## BURUNDI: TUNAO 'SAMATTA' WENGI

**Saada Akida na Adam Nyangasa, TUDARCo**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Burundi, Jimmy Ndayizeye, amesema haihofii Taifa Stars wala nyota wake Mbwana Samatta kuelekea mechi yao ya kirafiki ya kimataifa iliyopo katika Kalenda ya Fifa, licha ya kikosi chake kumkosa straika wao hatari anayekipiga Klabu ya ENPPI ya Misri, Fiston Abdoul Razak.

Timu hizo zitavaana Jumapili katika Uwanja wa Benjamini Mkapa, jijini Dar es Salaam, na jana Ndayizeye alitua nchini akiwa na wachezaji 10 ambao wataungana na baadhi wanaocheza Ligi Kuu Bara, huku wengine kutoka nje ya Burundi wakitarajiwa kuwasili hapa nchini leo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini jana, Ndayizeye alisema klabu ya ENPPI imemzuia nyota huyo kuja kuungana na wenzake katika mechi hiyo iliyopo kwenye Kalenda ya Fifa, lakini kukosekana kwa mchezaji mmoja au wawili hakutaathiri mipango yake kwa sababu Burundi wachezaji ni wengi ambao wanaweza kucheza nafasi yake.

**"Tumejiandaa vizuri hii mechi itakuwa ya kisasi kwa sababu Tanzania walituondoa katika makundi kipindi cha Afcon, hivyo hatutakubali kupoteza mechi hii ya kirafiki," alisema Ndayizeye.**

Alisema ana imani utakuwa mchezo mzuri wa kujipima nguvu kwa sababu anafahamu Tanzania na Burundi ni marafiki halafu viwango vya soka vinalingana.

"Kuhusu Samatta ni mchezaji mzuri, sitamhofia kwani katika kikosi changu kuna wachezaji ambao wanacheza nje, hivyo nina imani utakuwa mchezo mzuri na kiufundi zaidi," alisema kocha huyo.

9 770856 541002

**WAJE TU...**



Mshambuliaji wa Fenerbahce ya Uturuki na Nahodha wa timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta (katikati), akiwa na wachezaji wenzake mazoezini katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jana jioni wakati huu wakijiandaa na mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Burundi utakaopigwa Jumapili uwanjani hapo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# YANGA YASHUKURU DABI KUAHIRISHWA

## ●●●Simba watoa neno zito wakiigeukia Pan African na Mlandege, sasa yaiachia mtihani TFF...

**Na Saada Akida**

BAADA ya jana Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), kusogeza mbele mechi ya watani wa jadi, benchi la ufundi la Yanga linaloongozwa na Kocha Msaidizi, Juma Mwambusi, limesema ni jambo nzuri kwa sababu watapata muda mzuri wa timu yao kupata muunganiko mzuri kabla ya mchezo huo.

Mapema jana asubuhi taarifa ya TPLB kwa vyombo vya habari, ilieleza kuwa imefanya mabadiliko katika mchezo Na.61 wa Ligi Kuu ya Tanzania msimu wa 2020/21 kati ya Yanga na Simba uliokuwa uchezwe Oktoba 18 na sasa utachezwa Novemba 7, mwaka huu saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa mabadiliko hayo yametokana na uwezekano mkubwa wa kuwapo kwa vikwazo katika usafiri wa kimataifa baada ya kukamilika kwa michezo ya kimataifa iliyopo kwenye Kalenda ya FIFA, jambo ambalo linaweza kuathiri vikosi vya klabu hizo mbili. "Nchi nyingi bado zimeendelea kuweka masharti magumu katika taratibu za usafiri wa kimataifa tangu kuzuka kwa janga la virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19," ilieleza taarifa hiyo.

Lakini Nipashe lilipomtafuta Mwambusi jana kupata maoni yake kuhusu kusogezwa mbele kwa mchezo huo, alishukuru kwa kueleza kuwa mabadiliko hayo yatawasaidia kupata muda mzuri wa kukijenga kikosi chao pamoja na majeruhi kurejea katika hali nzuri.

Alisema hivi karibuni walikuwa na wachezaji wenye majeraha madogo madogo wakiwamo washambuliaji Michael Sarpong na Sogne Yacouba ambao wanaendelea na matibabu, hivyo hadi siku hiyo watakuwa fiti.

"Mabadiliko si mabaya kwa sababu kwa upande wetu, tunaendelea kujiimarisha vizuri, pia inatupa nafasi majeruhi wetu kuimarika vizuri na kuwa tayari kwa mechi hiyo.

"Kabla ya mabadiliko hayo tulikuwa tumejiandaa vizuri, nina imani mpira ni sayansi, kuna njia zake tungepata matokeo mazuri," alisema Mwambusi ambaye kikosi chake kilishaweka kambi kwa ajili ya mechi hiyo.

Kwa upande wa Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu alisema leo wanaanza programu yao baada ya hapo watakuwa na kikao na bosi wao, Kocha Mkuu, Sven Vandenbroeck kwa ajili ya kujadili mabadiliko hayo.

"Siwezi kusema lolote kuhusu mabadiliko hayo, kwa sababu nikiongea nitakuwa najisemea binafsi, kwa kuwa programu yetu inaanza kesho (leo), tunakutana benchi la ufundi na wachezaji, hivyo tukikutana na kulijadili hili naweza kutoa maoni yetu juu ya mabadiliko hayo," alisema Rweyemamu.

Lakini uongozi wa Klabu ya Simba uliopoulizwa kupitia kwa Ofisa Habari wake, Hajji Manara, ulisema hawana budi kukubaliana na mabadiliko hayo kwa kuwa wanaomiliki soka hapa nchini ni Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na TPLB, ambao wameona sababu ya kusogeza mchezo huo mbele.

"Kwa upande wetu Simba tunakubaliana na maamuzi ya wanaosimamia mpira ikiwamo bodi na TFF, kazi yetu sisi ni kucheza mpira na si upangaji wa ratiba, tumeyapokea hayo mabadiliko na tayari kikosi cha timu yetu kinaendelea na maandalizi ya mechi nyingine za ligi," alisema Manara.

Manara pia alisema wachezaji wa timu hiyo ambao hawapo na timu zao za taifa wataanza kujiandaa na mechi mbili za kirafiki dhidi ya Pan African itakayopigwa Oktoba 10, mwaka huu kabla ya siku nne baadaye kujipima tena nguvu dhidi ya Mlandege ya Zanzibar.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042